MADA:

# BONDE LA WAKATI KATIKA RIWAYA ZA KEZILAHABI:

NA:- BARU T. WAMBUI

"TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA '**MASTER OF ARTS**' KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI."

**JUNI 1992**

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0146275 3

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

## YALIYOMO


| | | UKURASA: |
|---|---|---|
| | Tabaruku | (i) |
| | Ungamo | (ii) |
| | Shukrani | (iii) |
| | Muhtasari | (iv) |
| **1:0** | **SURA YA KWANZA** | |
| 1:1 | Utangulizi | 1 |
| 1:2 | Somo la Utafiti | 2 |
| 1:3 | Madhumuni ya utafiti | 3 |
| 1:4 | Upeo na Tasnifu | 4 |
| 1:5 | Yaliyofanywa kuhusu Somo Hili | 5 |
| 1:6 | Haipothesia | 8 |
| 1:7 | Msingi wa Nadharia | 8 |
| 1:8 | Methodolijia | 11 |
| 1:9 | Tanbihi | 12 |
| **2:0** | **SURA YA PILI** | |
| 2:1 | Utangulizi | 14 |
| 2:2 | Ujadi na Athari Zake | 15 |
| 2:3 | Utamaduni wa Kigeni | 23 |
| 2:4 | Nafasi ya Dini Katika Utamaduni | 29 |
| 2:5 | Ujumbe wa Mwandishi | 32 |
| 2:6 | Kimalizio | 35 |


UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

**3:0 SURA YA TATU**

| | | |
|---|---|---|
| 3:1 | Utangulizi | 37 |
| 3:2 | Mfumo wa Elimu ya Kimagharibi | 38 |
| 3:3 | Ujumbe wa Mwandishi | 47 |
| 3:4 | Kimalizio | 49 |
| 3:5 | Tanbihi | |

**4:0 SURA YA NNE**

| | | |
|---|---|---|
| 4:1 | Uchumi na Jamii | 52 |
| 4:2 | Uchumi Katika Ujadi | 53 |
| 4:3 | Athari za kiuchumi-jamii | 56 |
| 4:4 | Kimalizio | 62 |

**5:0 SURA YA TANO**

| | | |
|---|---|---|
| 5:1 | Utangulizi | 64 |
| 5:2 | Athari za Mfumo wa Kibepari | 64 |
| 5:3 | Azimio la Arusha | 68 |
| 5:4 | Mapokezi ya Siasa ya Ujamaa | 71 |
| 5:5 | Kimalizio | 73 |

**6:0 SURA YA SITA**

| | | |
|---|---|---|
| 6:1 | Hitimisho | 75 |
| 6:2 | Unafalsafa wa Kezilahabi | 79 |
| 6:3 | Ukuaji wa Mwandishi Kifalsafa | 82 |

**MAREJELEO:** 85

TABARUKU:

Tasnifu hii nawatabarukia mume wangu, G. S. Wakoli, Mtoto wangu Sheila na Mamangu Regina Baru.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

## UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe
na haijatolewa kwa mahitaji ya
shahada katika chuo kikuu kingine."

BARU T. WAMBUI
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa
kwa idhini yetu kama wasimamizi
wa kazi hii, wa Chuo Kikuu
cha Nairobi."

PROF. JAY KITSAO

BW. MBATIAH, A. M.

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

## SHUKRANI:

Ufanisi katika kumaliza kazi kama hii ni matokeo ya usaidizi na kuungwa mkono na watu wengi. Sina budi kuwashukuru wote walionisaidia kwa namna moja au nyingine ili kuifanya kazi hii ifanikiwe.

Kwanza shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Profesa Jay Kitsao na Bwana Mbatiah A.M. Mashauri yenu ndiyo msingi wa kazi hii. Shukrani.

Nawashukuru pia wahadhiri wa idara ya isimu na lugha za Kiafrika kwa maoni yao bora waliyonipa mara kwa mara. Wahadhiri wa Kiswahili wakiwemo Bwana Kithaka wa Mberia, B. G. Mungania, Profesa Abdulaziz M. na Profesa Bakari nawashukuru kwa kunifunza.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu Florence, Wamitila, Swaleh na Yang kwa michango yao katika mijadala tulioshiriki pamoja na ambayo ilinifaa sana. Namshukuru Wamitila kwa maoni na misaada ya vitabu. Kamwe sitamsahau Florence, ambaye alinisaidia kuyatatua mawazo yangu wakati yalikuwa yamevurugika. Kwangu yeye alikuwa rafiki wa dhati.

Namshukuru mume wangu Sakwa Wakoli na mtoto wangu Sheila kwa mapenzi na kunivumilia wakati nilikuwa nikijitenga nao kwa sababu ya masomo. Mamangu mpenzi Bi. Regina Baru namshukuru kwa kunipa moyo wa kuendelea na kazi yangu.

Mwisho, namshukuru Bi. Joyce Macharia kwa kuipiga chapa tasnifu hii. Kwenu nyote Ahsante!

## MUHTASARI:


Tasnifu hii ni uhakiki wa riwaya nne za Kezilahabi yaani Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979), ukidhamiria kuchunguza jinsi ambavyo suala la bonde la wakati limemulikwa. Lengo kuu la tasnifu hii ni kuonyesha uzito uliopewa dhana ya bonde la wakati katika kuelezea mahusiano ya kijamii.

Imegawanyika katika sura sita. Katika sura ya kwanza kuna mada ya tasnifu, somo la utafiti, madhumuni ya utafiti, upeo wa tasnifu, yaliyofanywa kuhusu somo hili, msingi wa nadharia, haipothesia na mwisho methodolojia.

Sura ya pili inamulika utamaduni wa kijadi na ule wa kigeni. Nafasi ya dini pia imeshughulikiwa hapa.

Sura ya tatu inahusu mfumo wa elimu wa kimagharibi na jinsi inavyoathiri mtazamo wa kizazi kipya.

Sura ya nne inaziangalia athari za kiuchumi-jamii kwenye jamii.

Sura ya tano inahusu nafasi ya siasa katika kuathiri uhusiano wa wanajamii.

Sura ya sita ni hitimisho ambayo ni muhtasari wa yote yaliyojadiliwa. Katika sura hii pia kuna sehemu inayoangalia falsafa ya mwandishi na hatimaye sehemu inayozizungumzia riwaya za hivi karibuni za Kezilahabi yaani Nagona (1990) na Mzingile (1991)

## 1:0 SURA YA KWANZA

### 1:1 Utangulizi:

Dhana ya 'bonde la wakati' katika tasnifu hii itarejelea kwanza, vizazi viwili vilivyo na mitazamo tofauti kuhusu jamii, na pili, vizazi viwili vyenye umri tofauti. Kwa mfano kizazi cha vijana wa miaka kumi na mitatu na ishirini na tano, kitarejelewa kama kizazi kipya na ambacho ni kibadilifu. Nacho, kile cha wazee wa miaka arobaine na mitano na kuendelea, kitarejelewa kama kizazi kikongwe na ambacho pia ni kihafidhina.

Maudhui ya vizazi viwili ambavyo huwa na mielekeo tofauti ya maisha ni mojawapo ya vipengele vya fasihi vinavyojadiliwa na waandishi mbalimbali. Kumekuwa na mwelekeo wa kuoanisha migogoro itokeayo katika jamii na bonde la wakati. Mbali na tofauti za umri, masiala mengine kama vile athari za kimazingira, kwa mfano, elimu, mahusiano ya kijamii, siasa na utamaduni yamekuwa ni baadhi ya masiala muhimu yanayohusishwa na suala la vizazi viwili vyenye mitazamo tofauti ya maisha. Maudhui haya yanajitikeza sana katika fasihi ya ulimwengu, ile ya Kiswahili ikiwepo.

Katika riwaya ya Rosa Mistika (1971) iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi, kuna ukinzano kati ya Rosa na babake, Zakaria. Katika riwaya ya E. Hussein jambo hili limesawiriwa. Kwa mfano, katika Wakati Ukuta (1970) Tatu anakosana na mamake kuhusu suala la kutafutiwa mchumba. Jambo hili hili limesawihiwa na J. Kitsao katika tamthilia yake ya Uasi(1981) ambapo Riziki anakosana na babake Chande kwa kutaka kumwoza kwa mzee Nyamawi. Hii ni mifano michache tu.

Katika utafiti wetu tunataka kuona vipi na kwa nini tofauti za umri zinakuwa sababu ya mikinzano katika jamii na hivyo kusababisha kutengana kwa makundi haya mawili.

Isitoche, twataka kulitafiti swala hili katika fasihi ya Kiswahili na hatimaye kujua msimamo wa mwandishi Kezilahabi kulihusu. Mwishoni tutalitimisha kwa kutoa maoni yetu yatakayoungwa mkono na mifano ya waandishi wengine tuliowataja ili kupata msimamo hilisi wa kezilahabi kuhusu suala hili.

## 1:2 Somo la Utafiti:

Tasnifu itajishughulisha na uhakiki wa riwaya nne za Kezilahabi yaani Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979). Tutachukua kila mojawapo ya kazi hizi na kuchunguza jinsi ambavyo suala la bonde la wakati limemulikwa. Tunataka kuangalia chanzo na athari zake katika jamii.

Migongano kati ya baba na mwana kwa mfano, yaweza kuchukuliwa au kuonekana kama jambo la kawaida; lakini jambo hili litokeapo katika maandishi ya kifasihi lazima lichunguzwe kwa jicho la kutathmini. Hii ni kwa sababu katika maandishi ya kifasihi tunayojishughulisha nayo, kila jambo lazima lichunguzwe, lifikiriwe kwa makini na kupasiriwa ipasavyo.

Fasihi ni sanaa ambapo wasanii huchukua fenomena za kawaida katika jamii na kuzieleza upya. Hivyo hatupaswi kupuuza chochote kwa kuwa kile ni kitu cha kawaida mno katika jamii. Jukumu mojawapo la fasihi ni kuhimiza wasomaji na kudhihirisha ukweli wa matukio fulani katika maisha yao. Hivyo, fasihi haina budi kuwa chombo kiaminifu cha jamii hiyo. Ni lazima iwe na jukumu la kuieleza, kuichambua, kuikosoa na kiongoza jamii katika lengo lake la kuleta mabadiliko yafaayo ndani yake.

Samora (1977:28) anatufahamisha kwamba ujinga wa mtu mmoja ni udhaifu wa jamii nzima na huathiri kazi ya mmojawapo.

.../3

Anaendelea kusema kuwa, makosa ya mtu mmoja huifanya kazi ya kila mtu kuwa nzito zaidi, huhatarisha malengo ya jamii, na kuidhoofisha. Anawakumbusha waandishi wasione haya kuyataja makosa yanayofanyika katika jamii.

Hivyo, fasihi ni lazima iongoze umma. Iusaidie umma kutambua kuwa pengine maarifa yetu ya jana ni ujinga wa leo. Ni matumaini yetu kuwa tutaweza kuainisha mambo muhimu yanayosababisha kuendelea kupanuka kwa bonde lililoko kati ya kizazi kikongwe, ambacho tunakirejelea hapa kama hafidhina na kipya ambacho ni kibadhilifu. Tunataka kuangalia umuhimu wa athari ziletwazo na siasa, saikolojia, usomi na utamaduni wa kiafrika katika maendeleo na mabadiliko yake.

Isitoshe, ni jambo linalobainika kuwa leo kizazi kipya ni muhimu katika uundaji wa jamii mpya na iliyo bora zaidi. Katika jamii nyingi za kiafrika, kizazi hiki ndicho iletwayo na ukabila na hatimaye kujenga jamii mpya iliyo na misingi yake katika muungano halisi. Hivyo katika muktadha kama huu vizazi vyote viwili vyahitajiana katika nyanja zote za jamii na mifumo yote ya maisha.

Tukichukulia umri na tofauti za kimtazamo kuwa msingi wa kijelezi cha bonde la wakati, utafiti wetu utashughulikia uhusiano ulioko kati ya vizazi viwili muhimu hasa kipya na kikongwe na jinsi unavyojitokeza katika riwaya za kiswahili.

## 1:3 Madhumuni ya utafiti:

Lengo kuu la tasnifu hii ni kuonyesha uzito uliopewa dhana ya bonde la wakati katika kueleza mahusiano ya kijamii. Tunadhamiria kuonyesha kuwa kila kizazi kina nafasi yake

katika historia ya jamii yoyote ile na kwamba nafasi hii hutokana na tajriba kiliyo nayo kizazi chochote kile.

Utafiti wetu pia unanuia kuonyesha jinsi na kwa kiwango gani wasanii mbalimbali walivyoshughulikia swala la bonde la wakati. Tunataka kuangalia ukweli ulioko katika madai ya Musgroove (1964) kuwa, utengano na mikinzano itokeayo kati ya kizazi kubadilifu na kihafidhina, hutokana na sababu kuwa, kizazi kibadilifu kimo katika harakati za kuleta mapinduzi, yawe ni ya kisiasa, kitamaduni au kiuchumi, bali kizazi kikongwe hakipendelei mabadiliko. Tunaamini kuwa kwa kuzitalii na kuzihakiki riwaya za Kezilahabi, tutaweza kujitokeza na data ya kutosha kuyakanusha au kuyaunga mkono madai kama hayo.

Aidha tutajaribu kuonyesha msimamo wa Kezilahabi na baadhi ya mapendekezo yake katika kusuluhisha hali hiyo. Mwisho, twanuia kuthibitisha kuwa swala la migogoro iletwayo na bonde la wakati sio la kibiolojia au kisoshiolojia tu, bali ni mojawapo ya maudhui makuu yajitokezayo katika fasihi ya ulimwengu kwa jumla.

## 1:4 Upeo wa Tasnifu :

kama tulivyotaja, kazi yetu ni tahakiki na itahusu riwaya za Kezilahabi. Tutazichambua ili kuonyesha migogoro iletwayo na vizazi viwili vilivyo na mitazamo tofauti kuhusu jamii. Tunajua kuwa fasihi ya Kiswahili ni uwanja mpana sana, na kwa muda tulio nao, hatutaweza kuingilia fasihi nzima ya Kiswahili. Inatubidi basi kujiwekea mipaka. Utafiti wetu utalenga riwaya nne za Kezilahabi ambazo ni: Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979).

Mbali na riwaya, Kezilahabi amewahi kuandika mkusanyiko wa mashairi yaliyochapishwa katika kitabu cha Kichomi (1974) na Karibu Ndani (1988). Hatutazishughulikia kazi hizi mbili

za kishairi. Hivi karibuni, ameandika riwaya mbili Nagona (1990) na Mzingile (1991). Ingawa maudhui ya maana ya maisha yanaendelezwa hapa, hinsi na mwelekeo wake ni tofauti. Mwelekeo kuhusu maana ya maisha ni wa kifalsafa zaidi ukilinganishwa na jinsi unavyojitokeza katika riwaya zake za awali. Isitoche dhana ya bonde la wakati hai iashughulikiwa kama ilivyo katika riwaya nne za hapo awali. Kazi hizi tutazipitia katika sura ya mwisho tutakapozungumzia falsafa yake na maoni ya baadhi ya wahakiki wake kuihusu.

Ili kuweza kuipanua na kuipa misingi thabiti data yetu, tutagusia kazi za wasanii wengine kama vile E. Hussein, Wakati Ukuta (1970), J. Kitsao, Uasi na Cuthbert Oman, Mwenda kwao (1971). Kazi hizi na zingine zenye mwelekeo sawa zitatajwa kama mifano tu.

## 1:5 Yaliyofanywa kuhusu somo Hili:

Musgroove, F. (1964) anaainisha baadhi ya sababu zinazovifanya vizazi kuwa na mielekeo tofauti ya maisha. Anaziainisha data mbali mbali zilizopatikana baada ya utafiti kuhusu hisia za wahusika mbalimbali katika vikundi vyote viwili kukusanywa. Anasema kwa mfano kuwa, vijana wa umri wa miaka kumi na minne na kumi na mitano huwatenga watu wazima katika baadhi ya shughuli zao kuliko wanavyowafanya vijana wa umri sawa na wao. Kuhusu kizazi kikongwe, anasema kuwa utafiti ulionyesha kuwa ni cha watu wakaidi na huwashutumu vijana sana. Mwandishi huyu ni muhimu kwetu kwani anatuelekeza kwenye kiini cha tofauti za kihisia za vikundi hivi viwili.

Erikson, E.H. (1961) asema kuwa migogoro huzuka pale ambapo mzazi humdhamiria mwanawe avafanye tu yale ambayo yeye (mzazi) huona ni bora maishani mwake, na kuwa mwanawe

.../6

yuko pale kumtimizia haja zake maishani. Erikson anatusaidia kueleza ni kwa nini kizazi kikongwe hushindwa kutekeleza jukumu lake kwenye kilw kipya jambo ambalo hatimaye huibusha hisia za uasi kwenye kizazi kipya.

Ortega, Y. G. (1933) asema kuwa, kwa sababu ya tofauti katika mielekeo yao ya maisha, vizazi hivi viwili huwa na mikinzano. Hivyo kwake Ortega, tofauti ya wakati baina ya vizazi huwa ni kama kipimio cha kuchunguza tabia katika tajriba tofauti za binadamu. Vitabu hivi vinatuelekeza katika kuipambanua dhana ya 'vizazi' na kwenye sababu za mikinzano.

Kuhusu Kezilahabi Kiango, S.D. (1977) amejaribu kuonyesha mahusiano yaliyopo baina ya wahusika wa familia ya Zakaria. Hata hivyo makala yake ni mafupi na hayalengi kwenye uhusiano maalum wa ujana na uzee uliopo baina ya Rosa na babake Zakaria. Kiango amegusia kitabu kimoja tu cha Kezilahabi. Tutajaribu kuvuka mpaka kama huo.

Kitsao (1975) amegusia juu ya riwaya ya kwanza ya Kezilahabi Rosa Mistika. Amelishughulikia swala la maudhui kwa kiasi kidogo tu kwani tasnifu hii inahusu zaidi mtindo uliotumia kuziendeleza mbalimbali.

Vile vile Kitsao (1982) amegusia riwaya za mwandishi huyu. Hapa maudhui yametajwa kwa ufupi katika utangulizi. Hii ni kwa sababu kazi hii inaegemea zaidi upande wa mtindo wa takwimu. Tasnifu yetu itazama katika kipengee cha maudhui na hivyo kusuluhisha jambo kama hili. Kazi hizi mbili ni msingi bora wa maisha ya Rosa akiwa nyumbani, jambo ambalo latuelekeza kwenye sababu za mikinzano kati yake na babake.

Kazi nyingine inayoshughulikia maandishi ya Kezilahabi ni Mulokozi (1976). Makala haya yahusu uchambuzi wa riwaya tatu za Kezilahabi, yaani Dunia Uwanja wa Fujo (1975) Rosa Mistika (1971) na Kichwamaji (1974) makala haya yahusu zaidi maudhui ya kukata tamaa. Maudhui mengine kama vile

uhusiano kati ya vizazi tofauti hayajapewa uzito wowote, jambo ambalo twanuia kulijadili kwa upana wake.

Musau (1985) anapoihakiki riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo asema kuwa, baadhi ya maudhui makuu ya riwaya hii ya Kezilahabi ni 'fujo'. Hapo neno hili linaleta maana ya migogoro kati ya wazee wa kijiji na vijana ambao hawaafikiani kuhusu baadhi ya masiala yahusuyo jamii yao. Tasnifu yetu inadhamiria kuendeleza maudhui kama haya kwa kuonyesha kiini cha mwelekeo wa vijana au kizazi kipya katika kuyatatua masiala ya kijamii.

Lugano (1989) ameshughulikia mwanamke katika riwaya nne za Kezilahabi. Ameonyesha jinsi mwandishi huyu alivyowasawiri wahusika wake wa kike katika nyanja za siasa, nchini, elimu na jamii. Kazi yake inatuelekeza kwenye nafasi aliyopewa kila mwanajamii na jamii inayohusika. Kwa njia hii tunaelewa ni kwa nini inakuwa muhimu kuyagawa majukumu ya kijamii ili kuzuia kutoelewana baina ya wanajamii.

Habwe (1986) ameangalia maisha ya watanzania kama yalivyoathiriwa na mifumo mbalimbali ya kisiasa. Katika kulitalii swala hili amezingatia hali inavyojitokeza katika riwaya za Kezilahabi. Ameangalia jinsi mfumo wa ujamaa ulivyoanzishwa, kutekelezwa na athari zake kwenye wahusika mbalimbali. Hata hivyo hakuwahi kuonyesha athari za mfano huu katika kusababisha tofauti baina ya kizazi kipya na kikongwe. Pengo hili twanuia kuliziba.

Senkoro, F.E.M.K. (1982) amezungumzia riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo. Ameainisha baadhi ya maudhui yanayojitokeza katika riwaya hii. Maudhui ya vizazi yamegusiwa kwa ufupi tu. Ingawa ametuelekeza kwengye chanzo cha hali ya kutoelewana baina ya kizazi kipya na kikongwe, hakuwahi kulifafanua swala hili kwa upana wake. Tasnifu hii itaendeleza swala hilo na kulijadili kwa kirefu ikilinganisha na hali kama inavyojitokeza katika riwaya zingine za Kezilahabi.

Kuna mengi mengine yaliyoandikwa kuhusu riwaya za Kezilahabi. Hata hivyo tahakiki nyingi zimejihusisha na

maudhui mbalimbali na nafasi za wahusika ingawa hawakuwa na madhumuni ya kulizungumza swala la bonde la wakati.

## 1:6 Haipothesia:

Utafiti wetu utazingatia haipothesia zifuatozo:-

Kwamba katika riwaya za Kiswahili,

1. Utamaduni ndio msingi hasa wa migogoro inayosababisha bonde la wakati.
2. Elimu imemulikwa kama kiini muhimu kiletacho utengano unaosababisha bonde la wakati.
3. Siasa pia ni mojawapo ya kiini kinacholeta utengano unaosababisha bonde la wakati.
4. Masiala ya kiuchumi-jamii pia ni sababu kubwa ya migogoro inayosababisha bonde la wakati kupanuka zaidi.

## 1:7 Msingi wa Nadharia:

Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutatua au kutekeleza jambo fulani. Lengo la nadharia yoyote ni kumpa mhakiki vigezo vya kumwezesha kutoa maoni kuhusiana na kazi ya fasihi. Kwa mfano, anapoelewa nadharia inayoeleza fasihi yakinifu, anaweza kusoma fasihi yoyote na kutoa uamuzi iwapo mwandishi wa fasihi hiyo ametumia uyakinifu katika kuwachora wahusika wake na kama wahusika hawa amewaweka katika hali halisi ya kijamii.

Uhakiki tunaoufanya unahusiana na swala la jamii na fasihi, hivyo msingi wa kinadharia utufaao zaidi ni ule ujikitao katika uhakiki kijamii. Katika tasnifu hii tutaitumia nadharia ya uyakinifu wa kisoshiolisti unaoelemea

katika mtazamo wa Kimarx. Nadharia hii hutazama kazi yoyote ya sanaa kwa kuzingatia hali ya mazingira ya jamii inamozaliwa na kukuzwa sanaa hiyo.

Nadharia ya uyakinifu wa kisoshiolisti ina chimbuko lake nchini urusi. Dhana hii ilitumiwa awali na kina Stalin, Gorky na Zhdanov, katika miaka ya thelathini. Katika juhudi zao za kuleta waandishi chini ya utawala wa chama cha kikomunisti, chama cha RAPP* na vyama vingine huru vya waandishi vilivunjwa. Katika mwaka wa 1932, shirika la waandishi wa kisovieti liliundwa. Mnamo Agosti mwaka wa 1934 kongamano la kwanza la shirika la waandishi wa Kisovieti lilipofanya kikao chake cha kwanza, nadharia ya uyakinifu wa Kisoshiolisti, ambayo iliwahimiza waandishi kuwa ubunifu katika maandishi yao ni kiungo muhimu katika harakati za mapambano ya mja dhidi ya mazingira, ilitajwa rasmi kuwa mwongozo halisi katika kuendeleza maandishi ya Kisovieti.

Tangu nyakati za kikao hicho cha kwanza, uhakiki wa maandishi ya Kisovieti umetofautisha kati ya uyakinifu wa kisoshiolisti na uyakinifu wa kihakiki. Uyakinifu wa kisoshiolisti hurejelea fasihi ya Kisovieti kwanzia kwa maandishi ya Gorky, ambapo uyakinifu wa kihakiki huchukulika kama sifa bainishi ya waandishi wa ulaya na wa kirusi wa Karne ya kumi na tisa, ambao waliyachanganua mambo muhimu ya tamaduni za kisoshiolisti na Kidemokrasia katika jamii za kibwanyenye. Kazi za wahakiki-kisoshiolisti zilikuwa mfano wa umbuji wa hali ya juu na pia zilichukuliwa kama hati zilizoeleza kuibuka na kudhoofika kwa jamii za kibwanyenye. Kazi hizi zilihusu zaidi kusawiri mapambano kati ya tabaka la wanyonge na lile la mabwanyenye.

Uyakinifu wa kisoshiolisti kwa upande mwingine huchukulia kuwa maisha ni vitendo, ni ubunifu unaodhamiria kuendeleza uwezo alio nao binadamu wa kushindana na mazingira. Nadharia hii huzungumzia raha kuu ya kuishi ulimwenguni ambayo lazima

binadamu afanye awezalo kuilida ili kuweza kuishi kama muungano wa jamii moja ya kibinadamu. Hivyo, uyakinifu wa Kisoshiolisti hujishughulisha na matukio ya wakati ujao yaani yaelezea uundaji wa jamii mpya yenye furaha na iliyojengeka kwenye misingi ya kisoshiolisti.

Swali moja muhimu ambalo nadharia hiyo inauliza ni kama mwandishi asilia ameionyesha jamii yake kama ilivyo katika wakati fulani wa kihistoria. Akilishadidia jambo hili Ngugi wa Thiong'o (1978) anasema:

> Fasihi haikui na kuendelea katika ombwe tupu, inapewa nguvu, umbo mwelekeo na hata uwanja wa kushughulikia mivutano ya kijamii na mapito ya wakati ambayo yamesababisha kuvunjika kwa hali asilia ya jamii ile.[1] (tafsiri yetu)

Ukweli kuhusu maisha ya binadamu lazima ufahamike kwake na wenzake wote ili kwa pamoja waweze kuleta mabadiliko panapohitajika mabadiliko kwa manufaa ya jamii nzima. Jukumu hili ndilo linalosisitizwa na uyakinifu wa Kisoshiolisti.

Nadharia hiyo pia huuliza kama mwandishi asilia ana matumaini kuhusu hali ya siku sijazo za jamii yake katika kujiendeleza na kujiondoa kutokana na hali fulani. Kuhusu swala hili Lukačs (1962) anasema:

> Sanaa ya Kijamii haitosheki na mtazamo ulio halifu .... jukumu lake ni kuonyesha kuzaliwa kwa 'kesho' kutokana na 'leo' na matatizo yanayondamana na kuzaliwa huku.[2] (tafsiri yetu).

Lukačs anatupa mawazo mengi yanayofaa kuhusu muafaka uliopo kati ya sanaa na jamii toka enzi za kale hadi leo. Katika maelezo yake anaonyesha wazi kuwa sanaa inayo hali ya muendelezo ulio wa kipekee na muhimu; kwamba kwa kiwango

maalum sanaa ni wakili wa utu kadri inavyoafikiana na nyakati fulani za kihistoria. Dhana ya Uyakinifu wa Kisoshiolisti inamtarajia msanii auwasilishe uhalisi wa maisha katika hali yake ya kimaendeleo na kimapinduzi kikweli na kwa kuzingatia historia. Mikinzano yoyote ya kijamii huchangiza katika kuyaleta mabadiliko hayo.

Tukirejelea madhumuni ya tasnifu yetu twafikiria kwamba ni nadharia hii ya Uyakinifu wa kisoshiolisti itakayotufaa zaidi. Iwapo twatarajia kuonyesha uzito uliopewa mahusiano na maingiliano kati ya binadamu 'wanaoishi' katika enzi tofauti za historia ya jamii ile, basi hatuna budi kutumia kigezo kitakachodhihirisha kwa njia iliyo wasi jinsi msanii ahusikaye alivyoisawiri hali ile.

Tasnifu yetu pia yahusu migogoro inayosababishwa na vizazi viwili, kipya kinachoishi 'leo' na kile kikongwe kinachoishi 'jana'. Kiwakati nadharia ya Uyakinifu wa kisoshiolisti husisitiza uhusiano wa jana, leo na kesho. Ili kuifikia hiyo kesho, mkabala huu huonyesha mikinzano ya kijamii na asili yake, na hujitokeza katika uteteaji wa wanaonyanyaswa![13]

Uyakinifu wa kisoshiolisti husisitiza kuwa itikadi ya mwandishi haiwezi kutengana na sanaa. Sanaa yakinifu haijengeki kwenye itikadi zisizo yakini. Lazima itikadi ya mwandishi ionyeshe matumaini katika kuendeleza utu na imani kuwa binadamu aelewa na ukweli wa maisha. Hivyo msanii aliyejitwika wajibu wa kuichambua kazi ya sanaa kwa kuzingatia mtazamo wa Kimarx hana budi kuihakiki kazi hiyo kwa mujibu wa Uyakihifu wa Kisoshiolisti.

## 1:8 Methodolojia:

Uhakiki wetu utajikita katika maktaba. Tutajaribu kupekua tuwezavyo maandishi mbalimbali yanayohusiana na

uhakiki wa fasihi. Tutamhakiki kwa undani mwandishi tuliyemchagua E. Kezilahabi. Tutazinakidi riwaya zake nne yaani, Rosa Mistika, (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979).

Pamoja na riwaya hizi tutavisoma vitabu vya wasanii wengine wa Kiswahili ambao mawazo yao yanalandana au hata kukaribiana na kazi hii. Kwa sababu hii kazi kama vile uasi (1981), Wakati Ukuta (1970) Hatia (1972) na zinginezo zitatufaa sana.

Ingefaa tutaje hapa kuwa kazi tulizozitaja hapo juu zitatumika kwa kupanua mawazo tu. Zitatufaa katika kutuongezea mifano ya wahusika ambao wamo katika vizazi tofauti na wanakosana kwa sababu kadha. Kwa mfano tutaangalia vipi Hussein amelisawiiri swala la bonde la wakati katika Wakati Ukuta na sababu alizotupa kama kiini cha kuzorota kwa uhusiano baina ya Tatu na mamake.

Tutasoma pia maandishi na makala yanayohusiana na riwaya na fasihi kwa jumla. Maandishi haya ni kama tasnifu za wahakiki wengine ambao wamemhakiki Kezilahabi. Tahakiki kama hizi zitatufaa katika kutufunulia zaidi itikadi ya mwandishi wetu. Jambo hili litatusaidia katika kuujua kwa dhati msimamo wake kuhusu masiala yanayohusiana na aina ya jamii aliyoisawiri katika riwaya zake.

Mwisho tutazungumza na wasomi wenzangu pamoja na wataalamu wowote wale wanaoweza kutoa mawaidha mwafaka.

1:9 Tanbihi:

1. Ngugi wa Thiong'o (1978): Homecoming, Nairobi, H.E.B. uk. 65-66.

2. Lukais, G. (1962): <u>The Meaning of contemporary Realism</u>. London. The Merlin Press. uk. 25

3. Hapa dhana hii imetumika kurejelea kizazi kipya ambacho chahisi kuwa chaonewa na kile kikongwe. Hii yatokana na kuwa kizazi kikongwe kinatumia ujadi kuhakikia vitendo vya kizazi kipya ambacho kimekulia katika mfumo mgeni.

* RAPP - Muungano wa Waandishi wa kifanyakazi wa Urusi. (Russian Association of Proletarian Writers).

## 2:0 Sura ya Pili:

## 2:1 Utangulizi:

Ingwawa swala la mwingiliano wa tamaduni liliangaliwa na wasanii wa hapo awali kama vile Shakespeare, W. (1958) na Turgenev (1965), ni baada ya miaka ya sabini ambapo swala hili limepewa uzito katika fasihi ya Kiswahili.

Mitafaruku iliyosababishwa na mikinzano kati ya utamaduni wa kiafrika na ule wa kigeni uliorithiwa kutoka utawala wa kikoloni ilibainishwa. Misingi ya tamaduni za wafrika imeathiriwa baada ya kuingiliwa na athari mpya za maisha pamoja na kasumba za kikoloni. Jambo linalodhihirika ni kwamba ambapo kizazi kikongwe kinajaribu kubaki kimejifunga kwenye minyororo ya maisha ya jadi, kizazi kipya chaelekea kufuata mkondo wa utamaduni wa kigeni badala ya ule wao asilia.

Kupitia riwaya nne za Kezilahabi, yaani Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979), tasnifu hii yadhamiria kuthibitisha kuwa matokeo ya athari za kigeni yamesababisha mikinzano kati ya kizazi kipya na kikongwe. Utamaduni mpya umesababisha kuweko kwa ulimwengu usio na maafikiano katika jamii iliyokuwa imara na iliyojengeka kwenye misingi ya mila za jadi.

Yatupasa tutaje hapa ya kwamba, ingawa Kezilahabi ameyazungumzia masiala chungu nzima. Kama vile maana ya maisha, umuhimu wa ndoa, maadhili, dini na nafasi ya mwanamke katika jamii, taanifu hii itajikita katika kuliangalia suala la vizazi au maudhui ya bonde la wakati. Masiala mengine yatashughulikiwa tu pale ambapo

1. Mlacha, S.A.K. (1988) - Kiswahili - T.U.K.I. Juzuu 55/1 Uk. 45

yatasaidia kuyajengeka maudhui tunayoyashughulikia.

Katika sura hii tunakusudia kuonyesha jinsi mwandishi Kezilahabi alivyolisawiri swala la utamaduni katika riwaya zake tulizozitaja, na athari zake kwenye wanajamii kwa jumla. Katika kuliangalia suala hili tutaonyesha kuwa amali za utamaduni wa jadi na zile za kigeni zina mielekeo miwili tofauti. Moja yaelekea kuwa hafidhina ambapo nyengine ni badilifu. jambo ambalo hatima yake ni kutengana kwa kizazi kikongwe na kile kipya.

2:2 Ujadi na Athari Zake:

Ngugi wa Thiong'o (1972:4) anaueleza utamaduni kama mfumo mzima wa maisha ya watu wakiwa katika harakati za kutangamana na mazingira yao. Ni jumla ya sanaa, sayansi na amali zingine za kijamii ambazo ni pamoja na mfumo wa imani, itikadi na sherehe. Amali na sherehe zingine za jamii kwa kawaida huelezwa kupitia nyimbo, dansi za kitamaduni, sanaa ya uchoraji n.k. kupitia wakati amali na harakati hizi tofauti zimekuja kuashiria maana ya neno "utamaduni". Hivyo, miswada yoyote kuhusu utamaduni huwa inazungumzia haya lakini lazima tukumbuke kuwa miswada hutolewa katika hali ya maisha ya watu na hivyo hubadilika kulingana na mabadiliko ya maisha ya jamii.

Katika tasnifu hii tutachunguza sifa muhimu za utamaduni wa kiafrika katika hatua zake tatu za maendeleo ambazo ni: kwanza, kabla ya uvamizi wa wazungu, pili, chini ya ukoloni, na tatu katika hali ya kisasa mwafrika anapojaribu kuyamudu maisha yake.

Katika riwaya yake ya kwanza Rosa Mistika (1971), Kezilahabi anatuchorea maisha ya mhusika wake mkuu Rosa Mistika ambaye anaangamia kwa kushindwa kuyapatanisha malezi magumu aliyopewa na baba yake, na maisha ya mazingira

mapya. Maisha haya mapya yana misingi yake katika asasi zilizojengwa kwa misingi na utamaduni wa aina mpya yaani wa kigeni.

Rosa anazaliwa katika mazingira ya utamaduni wenye mielekeo ya kijadi. Utamaduni huu kama anavyosema Mwanyika (1978:62),

> Uliwafanya kuamini na kushikilia kuwa njia bora ya kujenga mtu katika tabia nzuri ilikuwa ni kujaribu kumwepusha mtu na mjaribu. Wengine walidiriki kuwaweka ndani wali wasionane na wavulana hadi mila itakaporuhusu wachumbiwe. Hivyo ndivyo Zakaria na Regina walivyojaribu kufanya katika kuwalea binti zao.

Kwa hivyo tunamwona Zakaria akijaribu kumchunga Rosa asipendane wala kukaribiana na wavulana. Juhudi zake zinafanana na zile za maksuudi mhusika wa S.A. Mohamed katika riwaya ya <u>Utengano</u> (1980), ambaye anajaribu kumtawisha bintiye Maimuna kwa kumtenga na jamii. Rosa kama Maimuna ananyimwa uhuru wa kujumuika na rika lake la wasichana na wavulana. Zakaria anasahau kwamba hali hii ya malezi ilifaa wakati wa kijadi na haitafaa kwa sasa.

Juhudi za Zakaria za kuwanyima binti zake kutangamana na wenzao, zatokana na fikra za kijadi kwamba wanawake wameumbwa ili waolewe na wapate watoto kwani mahali pao ni nyumbani. Hivyo basi, Zakaria anachelea kwamba binti zake watachezewa na wavulana kabla hawajafikia umri wa kuozwa. Hii ndiyo inayomfanya ajitahidi kuwafanya binti zake wawaogope wavulana. Juhudi zake zinadhihirika anapomwadhibu Rosa kwa kupokea barua na pesa kutoka kwa Charles. Tunaelezwa kuwa:

> Rosa alipigwa tena na tena,

> makofi yalikwenda mfululizo
> hata damu ikamtoka puani
> na mdomoni. Alilia, "Baba
> nihurumie, sitarudia tena,
> nimekoma". (UK. 12)

Jambo hili analirejelea anapowakaripia vijana waliokuwa wanatafuta mayai. Anawafukuza huku akiwacharaza viboko. Wanagadhabishwa na kitendo hiki na hivyo kumtukana(Uk.31).

Kwa sababu ya ukali wake, Rosa anaanza kuwa mnyamavu, mnyenyekevu na zaidi ya hivyo mwenye hofu ya kukaribiana na wanaume. Hali yake inafanana na ile ya Aurelia na Leonila katika <u>Dunia Uwanja wa Fujo</u> (1975) Mwandishi anatwambia kwamba:

> ...kasala aliwatunza kama maji
> ndani ya mtungi. siku moja alimpiga
> Leonila mpaka akazirai kwa sababu
> ya kukawia sana kisimani (Uk. 26).

Malezi haya chambilecho Musau (1985:22) yana msingi wake katika utamaduni wa jadi wa kiafrika. Utamaduni huo hauwarihusu walitafutiwa wachumba na wavulana. Wasichana walitafutiwa wachumba na wazazi wao. Malezi haya yanalingana na yale ayazungumziayo Hussein katika <u>Wakati Ukuta</u> (1971). katika tamthilia hii mama Tatu anamwambia binti yake,

> Mimi nimelelewa na wazee wangu,
> nilipokuwa mkubwa wakanipa mume.
> Sikumjua hakunijua, lakini mpaka
> sasa tunakaa vyema. Nami nita-
> kufanyia hivyo mpake nikupe nyumba
> yako.[2]

2. Hussein, E. (1971): <u>Wakati Ukuta</u> - Uk. 12

Malezi haya yameachwa nyuma na wakati unaobadilika. Hii yatokana na athari za kikoloni zilizoleta aina mpya ya utamaduni ulioandamana na mfumo mpya wa kielimu na kiuchumi. Wasichana kwa wavulana wanasoma pamoja shuleni ili kuyakabili mabadiliko yasiyo kuwa na budi kutokea. Mazingira ya shule yanawaruhusu wasichana na wavulana kuchangamana na kufanya urafiki. Hivyo, elimu inawapa vijana mtazamo wa mambo ulio tofauti na ule wa wazazi wao.

Hata hivyo Zakaria haoni mabadiliko haya. Mbali na udhaifu wake kama mzazi, anamlea Rosa kulingana na mila za jadi ambazo zimeachwa nyuma na mabadiliko ya kijamii. Chambilecho Kitsao (1975) yeye si mlevi wa pombe tu bali pia wa utamaduni na mila za kijadi za kiafrika.[3] Matokeo yake yanakuwa ni kile mwandishi anachokiita kwa kinaya "malezi mema." Hivyo, kukataa kwake kuyakubali mabadiliko ya kiwakati kunamfanya asimwelewe bintiye Rosa na hivyo kumshutumu kwa makosa yasiyo yake. Anamtarajia Rosa azifuate desturi za kijadi ilhali amezaliwa katika ulimwengu wa kisasa. Matokeo yake ni mikinzano kati ya baba na mwana na hatimaye chanzo kikuu cha bonde la wakati, chambilecho Musgroove:

> ...vijana wanapobaleghe wanakuwa
> na mielekeo tofauti na wazazi wao.
> Hali hii huibusha hisi za kikatili.
> baina yao kutokana na kuzingatia
> kwa amali tofauti.[4]

Zakaria anaendelea kuushikilia ukale kama afanyavyo Bibi Namtumaini katika Mwenda Kwao (1971). Rosa kama

3. Kitsao, J. - Tasnifu ya M.A. - UK. 147

4. Musgroove, F. (1964): Youth and the Social Order. Uk. 87

Stiri amevuka mipaka ya mila za kijadi na hivyo ana mtazamo tofauti kuhusu masiala mengi ya kijamii. Masiala ya ndoa na wachumba yamo mikononi mwa kizazi kipya na hivyo kizazi kikongwe hakina budi kuukubali uhalisi huu wa mambo. Wazazi wapaswa wasisahau kwamba hakuna utamaduni usiobadilika. Hii ni kwa sababu utamaduni ni kitu kilicho hai na huenda ukibadilika kulingana na mapito ya wakati. Isitoshe, utamaduni unaweza kujirekebisha kwa kufuata mahali na mazingira yaliyopo. Hii haina maana kuwa mazingira ya mahali yanazaa utamaduni wa aina fulani. Tunalokusudia ni kwamba ili utamaduni uweze kuishi na kujihifadhi kizazi hata kizazi, mwanadamu katika uhusiano wake na wenzake, maumbile na mazingira hana budi kuurekebisha utamaduni wake katika kila hatua ya maendeleo ya jamii yake. Huu ndio uhalisi wa mambo -kuishi sasa na kuyaangalia mambo kwa mitazamo inayowafiki.

Kwa mfano, kizazi jadi kinachoshikilia mila na desturi za zamani ni jamii ya wahafidhina, Ni sharti kikubali kwamba mabadiliko sharti yatokee katika jamii inayokabiliwa na athari ngeni za namna nyingi. Wasitumie mizani ya wakati uliopita kupimia matendo ya watoto wao.

Vijana nao wanapowakili 'usasa' wapaswa watambue walikotoka. Yaelekea Kezilahabi anatahadharisha dhidi ya kukataa asili yao kwa kung'ang'ania uzungu kwa jina la maendeleo, kwani hiki ndicho chanzo cha mgongano anaoueleza mwandishi.

Mikinzano kati ya mawazo ya kizazi kipya na kile cha jadi inadhihirika Kazimoto, Manase na bibiye wanapojadili utamaduni. Masiala kuhusu amala za utamaduni asilia yanapoibushwa hapa, mzee ambaye kwa sababu ya umri wake aweza kuchukulika kama baba yao wote anaingia. Kutokea kwake hapa kwasimamia mambo mawili: Kwanza, ni mzee ambaye amefanywa kuwatumikia vijana kwani ndiye mpishiwe Manase. Pili, anaingia wakati ambapo kizazi kipya kinajadili amali mpya, jambo ambalo lawakumbusha kuhusu mila na utamaduni wa kale.

Kitendo cha mkewe Manase kumkaripia mzee ni ishara ya

farka iliyoko kati ya kizazi kipya na kikongwe. Baada ya mzee kumwomba msamaha kwa kuchelewa, hata baada ya kueleza kuwa ni mkewe aliyekuwa mgonjwa, mkewe Manase anamjibu mzee huyu kwa kiburi na kutojali:

> Hadithi ya mke wako ... haituhusu sisi. Unapaswa kufika hapa saa kumi na moja. Umechelewa karibu sasa mbili nzima. Utakatwa mshahara. Kwanza mwezi huu umevunja karibu glasi tatu, hizo zitakatwa ... (Uk. 135)

Kudhoofikaa kwa uhusiano huu kunasimuliwa kwa undani na mwandishi anapotwambia:

> Mimi nilikaa kimya nikitazama kizazi kipya kikigongana na babu zake. niliona wazee wetu wanatuogopa. Nilianza kujiuliza kama hatuna lolote la kutegemea kutoka kwa wazee wetu isipokuwa kuwafanya wapishi, kuwakanyaga, kuwatisha na kuwakaripia (Uk.134)

Ingawa kisa hiki cha mkewe na mzee, mfanyakazi wao, chaweza kufasiriwa kwa njia tofauti, ni muhimu kionekane kama ithibati ya farka iliyopo kati ya wazee na vijana. Yaonekana kwamba vijana wanawadharau wazee. Hii yatokana na hali yao ya kufikiria kwamba mawazo yote ya wazee ni ya jadi. Hawalioni lolote bora kutoka kwa wazee na hivyo wanajifikiria kama kundi tofauti na lile la kizazi kikongwe na hili lasababisha kupanuka kwa bonde la wakati lililopo kati yao.

Suala la kufarakara kwa vizazi viwili vilivyo na mielekeo tofauti ya maisha pia twalishuhudia katika Dunia Uwanja wa Fujo (1975). Kupitia familia ya Kasala kwa mfano, mwandishi anatuchorea maisha katika kijiji cha Bugolola. Mfumo wa maisha unapobadilika, hali ya kiujima

inapungua. Kizazi kipya cha vijana kinataka uhuru zaidi wa kimapenzi, kiuchumi na kifamilia. Hii ni kwa sababu utaratibu mpya wa maisha haukubaliani na baadhi ya mila za kale. Vijana wanawatukana wazee bila kujali hatima ya kitendo kama kile. Utundu huu tunaushuhudia kati ya Misara na babake Kasala;

> 'Leo sichungi ng'ombe (O!'
> 'Utachunga!)Kasala alisema
> Kwa sauti kubwa.
> 'kila siku mimi nachunga, ninyi
> mnakaa tu! O!'
> 'Nikikushika leo utaona!'
> 'ukinishikaa!' Uk.5.

Katika utamaduni asilia wa jadi kila mwanajamii alitakiwa na jamii awe na uhusiano wa aina fulani na mwenzake. Uhusiano huu ulidumishwa kwa kaida zilizoongoza maisha na mienendo ya watu iliyokubaliwa na wote. Yeyote aliyekwenda kinyume cha desturi, asasi ilikuwa na njia maalum za kumuadhibu. Hali hii yaonekana imebadilika kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali, jambo ambalo limekuwa kiini kikubwa katika kuleta mafarakano kati ya kizazi kikongwe na kipya.

Swala la mikinzano kati ya vizazi linajidhihirisha pia katika riwaya ya Gamba la Nyoka (1979). Riwaya hii inahusu ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa nchini Tanzania. Mwandishi anaonyesha jinsi viongozi wa ngazi za chini wa sehemu hizo walivyojaribu kuwasukumia wakulima vijiji ambavyo walikuwa hawajaandaliwa kuvifahamu lengo lake.[5]

Jambo hili linazusha hali ya kutoelewana baina ya wanajamii wanaoishi kijijini na wale wa mjini ambao aghalabu ni wa kikazi kipya. katika hali ya kukataa maisha ya ya vijiji kunazuka vita na wanajamii kadhaa wanapoteza maisha yao hali wengine wanaumia.

5. Gibbe, A.G. (1982) - Kiswahili - T.U.K.I. Uk. 9

Katika mikutano mingi ya siri inayofanyika mistuni twaona kambi mbili za jamii katika ubishano. Wazee na vijana wanapotoa maoni yao kuhusu suala la kuhamia mijini wanaonekana kutokubaliana. Vijana wanapopewa nafasi ya kusema wazee wanaonelea kwamba jambo hili halifai. Hili ladhihirika katika jinsi wazee wanavyoliangalia swala la kuhamishwa mijini kama kitendo cha vijana walioelimika. Katika mkutano, wazee wanachukulia kitendo cha vijana kuzungumza mbele yao kama muhali. Wanakiona kitendo kisichofaa kwani hawasemi lolote la maana 'wanabwatabwata' tu mbele yao. Wazee, katika kushikilia itikadi za kijadi kuwa uzee ni busara hawaoni maana yeyote kushauriwa na vijana, kwani sikio haliwi refu kuliko bega (uk.17). Huu ni mfano mzuri wa wazee wanaokimbia ukweli wa mambo kuwa utamaduni hauna budi kubadilika.

Katika kutuonyesha kiini cha mikinzano kati ya kambi hizi mbili, yaani kizazi kikongwe na kipya, mwandishi ametuchorea wahusika ambao amali zao zinapingana kabisa. Kasumba ya 'usasa' imewakumba kina Kazimoto, Manase, Anastasia, Tumaini na Dennis kiasi cha kutoafiki hata kidogo wanayoshikilia Mungere, Kasala na wengine katika kizazi kikongwe. Ukweli wa mambo kama unavyojidhihirisha hapa ni kwamba ingawa binadamu ana uwezo wa kubadilisha mazingira na mfumo wake wa maisha, hana uwezo wa kubadilisha wakati.

Migongano baina ya kizazi kikongwe na kipya pia imejitokeza katka fasihi nyingine ya Kiswahili. katika tamthilia ya J. Kitsao iitwayo Uasi (1980), Riziki ambaye ni msichana aliyeelimika adhamiriwa kuozwa kwa mzee nyamawi, na babake Chande maadam atapewa mahari nono. Maneno ya Riziki yanapiga mwangwi maneno ya vijana wengine kama vile Kazimoto, Tumaini na Tatu, Maneno yake yanaonyesha uhalisi wa maisha anaposema:

> Wakati wa wazee kuwachagulia
> waume binti zao na wake
> watoto wao wa kiume umeshapita.(Uk.27)

Kuhusu suala hili John mhusika mwingine anasema:

> Kitu cha busara cha sisi kufanya sio tu, kumnyakua Riziki kutoka mikononi mwa babake Kesi, bali vile vile kuionyehsa hii mijizee kuwa wakati umebadilika na kwamba kwenye mambo ya posa na ndoa wazazi huwa washauri tu. Hiari ya kuolewa huwa ya msichana mwenyewe.[6]

Hatima ya migongano hii ni kutoroka kwa vijana, kama inavyojitokeza katika Dunia Uwanja wa Fujo (1975), Wakati Ukuta (1970) na Uasi (1980). Waandishi wanawatorosha vijana kutoka nyumbani wakati inapobainika kwamba fikra zao kuhusu maisha ya kisasa haziambatani na misingi ya wakati wa jadi uliojikita katika kujihifadhi na unaohitaji kubadilishwa ili watu waweze kuelewana.

Katika sehemu hii tumeona jinsi elimu au malezi katika ujadi yamemulikwa na mikinzano kati ya kizazi kikongwe na kile kipya. Ingawa tungetarajia wazazi waweze kuwalea watoto ipasavyo ili kuwe na utangamano katika jamii, mwandishi aelekea kuwashutumu wazazi kwa kutumia kaida za utamaduni mkongwe kupimia matendo ya wana wao. Katika sehemu inayofuata tutaangalia ni kwa kiasi gani utamaduni wa kigeni umemulikwa kama kiini katika kusababisha mitafaruku kati ya kizazi kikongwe na kipya na hivyo kusababisha bonde la wakati.

## 2:3 Utamaduni wa Kigeni

Ukoloni ulipojipenya kwenye jamii za wafrika ulizua kasumba ya mwafrika kujidharau na kumtukuza mkoloni.

6. Kitsao, J. (1980): Uasi - Uk. 28

.../24

Mwafrika alitekwa kabisa na ukoloni jambo ambalo lilikuwa na athari kubwa kwa wale ambao ama walikuwa chini ya ukoloni au wapo chini ya ukoloni mambo - leo. Akiliweka wazi jambo hili Frantz Fanon anasema:

> ... kila jamii inayotawaliwa,
> kila jamii ambayo katika roho
> yake mmeota kasumba ya mawazo
> ya kufugwa iliyosababishwa
> na kutekelezwa kwa utamaduni
> wake wa asili, punde hujikuta
> imekabiliana na lugha na
> utamaduni wa taifa linalodai
> kuwa limekuja kulistaarabisha.
> Hadhi ya mtu anayetawaliwa hupanda
> na ushenzi wake hupungua kwa
> kadiri anavyofaulu kuigiza utamaduni
> wa mtawala wake, ushenzi wake,
> ndivyo kadri anavyokaribia uzungu.[7]

Ukweli wa kauli hii umejidhihirisha katika riwaya za Kezilahabi. Wahusika wakuu katika riwaya zake ni vijana ambao kwa upande mmoja ni wanachama wa jamii mpya na kwa upande mwingine wamo katika kipindi ambacho wanajenga familia zao. Nguvu hizi mbili zinawatenga na tamaduni zao za jadi ambazo zinawachukulia kama wanachama wasiopevuka na ambao wamo chini ya ulinzi na uongozi wa wazee waliopevuka. Haja ya uhuru unaochochewa na utamaduni wa kigeni unamulikwa kama kiini muhimu cha mkinzano na uongozi wa wazazi unaotekelezwa kijijini na unaoathiriwa zaidi na utamaduni asilia.

Katika <u>Dunia Uwanja wa Fujo</u> (1975) kwa mfano, mwandishi anayasawiri maisha ya vijana kama vile Tumaini, John na Anastasia ambao wanatoroka kijiji na kwenda kuishi mjini. Ingawa hatwambii mengi kuhusu wahusika wengine, maisha ya vijana hawa yaonyesha kuweko kwa uhuru kutokana na mamlaka

7. Frantz, F. (1970): <u>Black Skins White Masks</u> Uk. 14.

ya kijadi hadi kufikia kiwango cha kuimarisha matakwa yao kwenye kizazi kikongwe.

Katika jamii za kijadi vijana walielewa kwamba, wapaswa kuwa na tabia njema na ifaayo kulingana na nafasi waliopewa na jamii. Mafanikio ya wakati ujao yalitegemea kuelewa kwao nafasi waliopewa katika jamii, kuonyesha heshima na utiifu ilipohitajika. Majukumu ya kijamii yalipangwa na kutofautishwa kulingana na mfumo wa kugawa wanajamii katika makundi mbalimbali kulingana na umri. Hii ilinuiwa kudumisha uhusiano mwema kati ya makundi ya wanajamii wote. Hali hii ndiyo twaishuhudia ikiporomoshwa na majilio ya mfumo wa kikoloni ulioandamana na utamaduni mgeni.

Mgongano wa aina hii unaonekana katika tabia mbalimbali katika <u>Kichwamaji</u> (1974). Huu upo hasa kati ya mila za kijijini zilizoambatana na jadi za kikabila na utamaduni wa mjini ulioambatana na njia mpya na ngeni za maisha. Mwandishi aelekea kutueleza kuwa sababu ya kutengana kwa kizazi kikongwe na kile kipya ni baadhi ya tabia zilizoibuka katika kizazi kipya baada ya kuathiriwa na utamaduni wa kigeni.

> Mimi nilikua peke yangu ..... nilijiona nimo katika hali ya upweke. Nilijiona kama mtu mchoyo niliyejitenga ... Niliona kiini cha mambo haya yote. kati yangu na wale waliokuwa wakila juu ya sakafu niliona ukuta mrefu - mila (uk.180).

Wakati kazimoto anapomtembelea rafiki yake Manase na mkewe, hapo ndipo tunapotambua mgongano na mwingiliano wa tamaduni waziwazi. Manase, kazimoto na Salima wanawakilisha kizazi kipya kilichoundwa na kuathiriwa na mambo mapya na mengine mageni. Manase na Kazimoto wanapoongea juu ya muziki, Manase anaonyesha kupenda nyimbo za kigeni zaidi

kuliko za Kiafrika. Huku ni kutawaliwa kiutamaduni na kimawazo hadi kiwango cha mtu kujichukia mwenyewe. Picha tunayopewa juu ya chumba cha Manase inasisitiza jambo hili. Tunaambiwa:

> Mambo niliyoyaona humo chumbani yalikuwa kama haya: Rediogramu kubwa kama meza, makochi na meza kati kati iliyokuwa imepambwa na kitambaa cheupe; juu ya meza niliona ubao wa 'chess' na vipande vyake. Sakafu yote ilikuwa nyekundu. Kuta zilikuwa na miigizo ya picha zile zilizochoma na kina Raphael na michelangelo. (uk.132).

Mbali na kuwa jumba hili twaliona kuwa la anasa sana hasa tunapolinganisha na nyumba kama za kina Moyokonde na vumilia, nyumba yenyewe ni kioo cha utamaduni wa kigeni. michezo yake Manase ni 'chess', picha zake ni za kina Raphael na Michelangelo. Muziki wa kongo au Afrika Mashariki hana bali ana rundo kubwa la sahani za santuri za nyimbo za nje ambazo anasema kuwa zina uzito wa mawazo na wa sanaa zaidi ya zile za kiafrika zinazolia mbu mbu mbu tangu mwanzo hadi mwisho, kiasi cha kuleta hata mbu ndani ya nyumba. (uk.133)

Wakati wa sherehe za arusi ya kazimoto na Sabina jambo hili linajitokeza tena. Twaelezwa kwamba:

> Ngoma za kienyeji zilichezwa na watazamaji walitoka katika kijiji mbalimbali. Walimu na maofisa kadhaa walivua mashati yao na kucheza ngoma. Hawa ndio walio-chekesha watu wengi, na wengi walikimbia kwenda kuwatazama (uk.167)

Swali ambalo hatuna budi kuuliza ni, kwa nini walimu na maofisa wachekeshe watu wakati wakicheza ngoma ambazo ni za utamaduni wao? Jibu ni kwamba walimu na maofisa wanaonekana kuwa kichekesho kwani ngoma hizi zimekuwa si za watu wakubwa na waliosoma. Wao sasa ni kama wakubwa na wanakuwa kichekesho kama vile ambavyo mzungu atakuwa kichekesho akijiunga na Sindimba[8].

Tabia za watu zimebadilishwa na mfumo mpya uliotokea katika jamii. Kuwapo kwa matabaka ya 'wanasasa' kumefuta kabisa tabia za kijadi. Wazee sasa ndio wanaowatetemekea na kuwaheshimu vijana. katika nyakati za jadi tusingetazamia watu kama kina salima kumkemea mzee wa umri kama ule wa mfanyakazi wao pale nyumbani, kama alivyofanya mkewe Manase. Ingawa mabadiliko katika utamaduni yanasababishwa kwa kiasi kikubwa na athari za utamaduni wa kigeni, hatuwezi kutenga uwezekano kuwa mfumo wa kijadi umeonyesha ukali mwingi katika kudumisha ukale na kutopendelea mabadiliko jambo ambalo halisaidii kuhimili uhusiano mwafaka kati ya wazee na vijana.

Katika Rosa Mistika kwa mfano, Rosa anaubadilisha mtazamo wake kuhusu maisha anapotoka katika mamlaka makali ya wazazi wake. Anapojiunga na shule anajipata katika mazingira tofauti kabisa na ambayo yanayapinga yale aliyojifunza nyumbani. Ni mitazamo halifu ya wanafunzi wenzake wavulana kwa wasichana, walimu na maofisa wa serikali kutoka mjini inayokuwa kiini muhimu katika kubadili mwelekeo wake Rosa kuhusu alivyojielewa na kuielewa jamii yake ya kijadi.

Kwa mfano baadhi ya mambo yanayoendelea shuleni ni yale ya starehe na anasa. Dansi ni mojawapo. Tunaelezwa:

> Rekodi inawekwa na sanduku linatoa
> sauti. Mara moja wavulana wanaamka
> kwenda kuinama; miungu wadogo wanaweka

8. Senkoro, F.E.M.K. 91976): Kiswahili - T.U.K.I. Uk. 90.

> mikono yao kifuani kuonyesha kwamba wanakataa. Wengi wanakubali. Huu ni wakati wao wa umalkia. Hapa mvulana mmoja mwenye suti anamwinamia msichana, msichana anakataa, lakini anapotega mgongo msichana anachukuliwa na mvulana mwingine ambaye hana hata tai... Ni ajabu mambo yanvyocndcshwa humu ndani. (uk. 39).

Starehe kama hizi zina misingi yake katika utamaduni wa kigeni. Mambo haya yanaleta maingiliano kati ya wasichana na wavulana, ambayo mwandishi ayaona kuwa 'hatari' hasa kwa vijana kama Rosa ambao hawana ujuzi wa maisha kama yale. Kutokana na uhuru waliopata kutokana na utamaduni wa kigeni kizazi kipya chaelekea kimechukua hatamu za 'uongozi' mbele ya kile kikongwe. Katika utamaduni jadi wavulana na wasichana waliruhusiwa kukutana katika ngoma na michezo mbalimbali iliyoluhusiwa na kusimamiwa na jamii. Jambo hili liliwapa fursa ya kukutana bila kuwepo uhuru unaowapa nafasi ya kufanya vitendo vya izara.

Kilele cha mikinzano kati ya Rosa na babake chatukia wakati Kamshina wa Wilaya anapofika nyumbani kumchukua Rosa. Rosa na babake wanagombana hadi kufikia kiwango cha baba kumkana binti na binti kumkana babake.

> Rosa, tangu leo wewe si mtoto wangu. Tangu leo wewe si baba yangu. (uk. 69-70).

Katika maneno ya vizazi hivi viwili twashuhidia kilele cha mgongano kati ya kambi hizi mbili zenye mielekeo tofauti kuhusu jinsi ya kuyaendesha maisha. Hata ingawa mgongano huu una sehemu katika malezi ya jadi (kunyimwa uhuru), twaona kwamba tabia ya Rosa na kushiriki kwake katika ugoni kwatokana na hali ya maisha anayoshuhudia shuleni. Mitindo mipya ya maisha ya mjini na athari za vijana marafikize inakuwa ni kiini kikubwa kinachochangia kubadilika

..../29

kwa mwelekeo wake kuhusu maisha na hatimaye kukosana kwake na babake.

Katika sehemu hii tumeona jinsi utamaduni wa kigeni ulivyojipenya kwenye kizazi kipya na kukiathiri kiasi cha wao kujihisi kuwa wanaweza kuchukua hatamu za uongozi. Utamaduni huu umeibusha hali ya kujihisi 'huru' na hivyo kuwa na uwezo wa kuyafanya yote yaliyoonekana muhali katika utamaduni jadi. Katika sehemu ifuatayo tutaichunguza asasi ya dini ambayo ni mojawapo ya asasi muhimu katika utamaduni wa jamii yoyote ile. Twataka kuona vipi dini inachangia katika kufarakanisha kizazi kipya na kile kikongwe na hivyo kulipanua zaidi bonde la wakati.

## 2:4 Nafasi ya Dini katika Utamaduni:

Omari na Mvungi (1981) wanaieleza dini kama ule mfumo wa itikadi na matendo, vitu ambavyo hueleweka na hutambulika kwa njia ya imani na si kwa njia ya utafiti wa kitaaluma. Zaidi, dini lazima imhusianishe mwanadamu na mungu au viumbe wengine waishio ambao huaminika kuwa wanayo mamlaka kuliko wanadamu, ya maisha baada ya kifo na ulimwengu ujao; mambo ambayo hayafahamiki kitaaluma, kitafiti au kutawaliwa nayo.

Kama inavyojulikana miongoni mwa wana elimu-jamii, dini ni mojawapo ya asasi kama vile shule, familia na marafiki ambazo huwafunza watoto au watu kwa jumla ili waifae jamii yao. Inaaminika kwamba dini inaweza kuiathiri tabia ya wanajamii.[9]

Katika Rosa Mistika dini inawakilishwa na Padri anayemjia Rosa chumbani mwake katika chuo cha Ualimu, Morogoro. Inawakilishwa pia na masista wanaosimamia shule ya Rosary. Kabiliano la ana kwa ana la Rosa na dini ni

9. Mckee, J. (1969): Introduction to Sociology Uk. 393.

pale anapokutana na Padri. Ni ajabu kwamba Padri haonekani kuielewa hali ya maisha ya Rosa. Yeye anachukulia ya kwamba bibilia ndiyo suluhisho. Anazungumzia mambo ya kidhahania ambayo hayawezi kumsaidia. Mwandishi asema:

> Kama Padri angalizungumzia juu
> ya mambo haya (yanayomsumbua)
> labda angeliweza kumsaidia.
> Lakini yeye alianza kuzungumzia
> juu ya wokovu. (Uk.58).

Ni bayana kwamba Padri haelewi kiini cha tabia ya Rosa. Hivyo analenga pasipo, katika juhudi zake za kumsaidia. Hili linamfanya Rosa kumuuliza;

> .... kwa nini wewe ujali roho
> yangu kuliko mimi mwenyewe? (uk. 59)

Kwa kukosa jibu mwafaka Padri anamfokea na kumwita 'Lusifa'. Dini imeshindwa kutekeleza wajibu wake - wa kumwongoza Rosa na 'kuichonga' tabia yake ili aweze kuishi kwa njia ifaayo.

Padri ambaye amepewa mamlaka ya kuziongoza roho za wanajamii, aweza kuwekwa katika kikundi kimoja na masista au walimu wa shule ya Rosary. Ingawa twamtarajia kuwa mtu aliyesoma, anakosa kufahamu jinsi malezi ya babake Rosa na mazingira anamojikuta yanavyoathiri tabia yake. Isitoshe dini inashindwa kumsaidia Rosa kwa jinsi inavyomzingatia maisha ya mbinguni kuliko ya hapa duniani. Tunamwona Padri akimhubiria Rosa kuhusu wokovu na ufalme wa mbinguni. Katika mazishi ya Rosa, Padri analikariri wazo hilo anaposema:

> Ee Mungu, viumbe vyote vinaishi
> kwako, na miili yetu inapokufa
> haipotei bali hugeuzwa kuwa
> bora zaidi. (uk. 114).

Yaelekea Padri anaukimbia uhalisi wa mambo. Ukweli ni kwamba, Rosa alikuwa na matatizo yaliyomsumbua sana ambayo kiini chake kilikuwa ni malezi finyu aliyopewa akiwa mchanga. Kinyume na mawazo ya Padri, nadharia ya uyakinifu wa kisoshiolisti huzumgumzia raha kuu ya kuishi ulimwenguni ambayo lazima binadamu afanye awezalo kuilinda ili kuweza kuishi kama muungano wa jamii moja ya kibinadamu. Kwa kuwa Padri haonekani kuyajali haya, Rosa anahamaki jambo ambalo linasusha kutoelewana kati yao. Mwandishi atueleza kwamba hakuzidi kumwona tena. Kutokana na kutoelewana huku dini inakuwa kiini cha mgongano kati ya Rosa na Padri.

Nafasi ya dini imejitokeza pia katika riwaya ya Kichwamaji. Katika majadiliano kati ya kazimoto na wazee, kazimoto anatoa maoni kwamba huenda hakuna Mungu:

> Mambo yaliharibika nilipoanza
> kuwaambia kwamba wote walikataa
> kabisa. Mzee mmoja aliinuka
> kwenda nyumbani. (uk. 59).

Yaonekana kwamba kizazi kipya hakina imani na dini katika jinsi inavyoshindwa kutatua shida zinazotokea ulimwenguni. Kama tulivyotangulia kusema hii yatokana na sababu kwamba masiala ya kidini hayaelezeki kwa njia ya elimu-utafiti. Kutokana na maoni yao tofauti kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu, vizazi hivi vinaishia kutoelewana kama tunavyoshuhudia katika jinsi wazee, wanavyomtukana kazimoto wakimwita 'mwehu'.

Hivyo, mwandishi aelekea kutwambia kuwa badala ya dini kuwa suluhisho la kuziba ufa ulioko baina ya kizazi kikongwe na kile kipya, inakuwa kiini cha utengano nao. Haya twayaona katika jinsi vizazi hivi vinavyoangalia masiala yahusuyo maisha kwa mielekeo tofauti.

2:5 Ujumbe wa Mwandishi:

Katika kutuonyesha jinsi utamaduni wa jadi, wa kigeni na dini inavyokuwa kiini cha mitafaruku kati ya vizazi viwili vilivyo na mitazamo tofauti, mwandishi ametuchorea wahusika wa kambi hizi mbili na jinsi wanavyotengana.

Kezilahabi aelekea kutuambia kwamba, mwelekeo wa kijadi kuhusu maisha hausaidii katika kujenga maadili ya vijana. Vijana wanakua katika wakati wa sasa ambao ni tofauti na wa zamani, kwa sababu ya maingiliano ya jamii mbalimbali. Maingilaiano haya yameleta kuathiriana kwa tamaduni mbalimbali ambako kumezusha matatizo tofauti na yale ya jadi. Kwa hivyo kuna haja ya kuweka mbinu mpya ambazo zitakuwa mwafaka kwa hali ya maisha ya kisasa.

Tumeona kuwa utamaduni hauna budi kubadilika kulingana na wakati. Hivyo, katika harakati za kuyamudu mazingira yao wanadamu, huunda mapya na kwa kufanya hivyo hubadilisha pia mfumo wao wa maisha na fikra. Kule kung'ang'ania 'ujadi' kwa mfano, na kizazi kikongwe, ni sawa na kupigana na wakati. Ukweli ni kwamba wakati ni ukuta na mwanadamu anapojaribu kushindana nao hatima yake itakuwa kuleta madhara kama tulivyoona katika kurasa za awali. Mikinzano baina ya vizazi viwili, kikongwe na kipya ni baadhi ya matatizo hayo.

Kiwakati, nadharia ya uyakinifu wa Kisoshiolisti husisitiza uhusiano wa jana, na leo na kesho. Ili kuifikia kesho mkabala huu huonyesha mikinzano ya kijamii na asili yake na hujitokeza katika uteteaji wa 'wanaonyanyaswa'* Wazazi ndio wanaotegemewa na jamii kuwajenga vijana kitabia, walakini, kama tunavyoona, wao wenyewe ndio wanaokuwa chanzo cha kuharibika kwa vijana hao.

* Neno hili hapa linatumika kwa maana ya kizazi kipya, kinachoshikilia kwamba kizazi kikongwe 'kinakidhumu' kwa kukinyima haki yake - uhuru wa kuyatazama masiala ya kijamii kwa mielekeo mipya na tofauti na ile ya kizazi kikongwe.

Mwandishi aelekea kutwambia kwamba hali hii ya vijana kukosa maadili yanayofaa katika jamii itaendelea iwapo watakosa kupewa malezi mema kama anavyosema Chacha (1978:106).

Kwa kutubainishia malezi yanayotolewa nyumbani mwandishi analenga katika kuumulika udhaifu wa mwelekeo wa kijadi. Malezi yaliyo na misingi yake katika utamaduni wenye mielekeo ya kijadi yanashindwa kuwaelekeza vijana kwa mwelekeo huu unapingana na mwelekeo mpya katika maisha yao. Ni jambo la kushangaza kwamba Zakaria na kapinga wanapowaadhibu binti zao hawawaelezi ubaya wa kutangamana na wavulana. Kitendo hiki kinaenda kinyume na uhalisi wa hali ya maisha.

Isitoche mambo kuhusu mahusiano ya wavulana na wasichana hayashughulikiwiipasavyo. Hii ndiyo sababu tunapata visa vingi vya wasichana na wavulana wakiyaingilia maisha ya uzinifu bila tahadhari yoyote. Vitendo vyao vinachukuliwa na kizazi kikongwe kama vitendo vya uasi. Jambo hili ndilo linalosababisha kutengana baina ya vizazi hivi na hivyo kupanuka kwa bonde la wakati. Jambo hili lingesuluhishwa kama kila kikundi kingalijitahidi kukielewa kama kila kikundi kingalijitahidi kukielewa chenzake.

Kuhusu swala la dini na dhila yake katika kuleta mahusiano na uelewano mwafaka kati ya wanajamii, mwandishi aonelea kwamba imeshindwa. Katika <u>Rosa mistika</u> twaona jinsi kiongozi (Padri) anavyoshindwa kumsaidia Rosa kwa sababu hazingatii kiini cha matatizo yake.

Aonekana kufikiria kuwa matatizo yake yatokana na udhaifu wake mwenyewe. Wazo hili lajitokeza wakati wa mazishi ya Rosa na wazazi wake. Padri anaomba hivi:

> ...twakuomba sana kwa wema na
> huruma yako uzirehemu roho za
> watumishi wako na kuyafuta
> makosa yaliyowapata walipokosa
> kutimiza mapenzi yako kwa
> hila za shetani na kwa
> ubaya na udhaifu wa wenyewe (uk. 114).

Yaelekea haifahamu nafasi ya malezi katika mazingira yaliyoathiriwa na utamaduni jadi yanavyosaidia kuiharibu hulka ya vijana kama Rosa.

Padri anapomhubiria Rosa kuhusu wokovu na ufalme wa mbinguni, aonekana kuukimbia uhalisi wa maisha. Hivyo dini inapuuza maisha halisi ya hapa duniani. Inafikiria ya kwamba maisha ya mbinguni ni bora zaidi kuliko yale ya ulimwengu huu. Ukweli wa kauli hii unaungwa mkono na nadharia hii huchukulia kuwa maisha ni vitendo. Ni ubunifu unaodhamiria kuendeleza uwezo alionao binadamu wa kushindana na mazingira. Kinyume na mwelekeo wa dini, nadharia hii huzungumzia raha kuu ya kuishi ulimwenguni ambayo lazima binadamu afanye awezalo kuilinda ili kuweza kuishi kama muungano wa jamii moja ya binadamu. Hivyo, ingawa binadamu ana uwezo wa kubadilisha mazingira na mfumo wako wa maisha, hana uwezo wa kubadilisha wakati.

Mwandishi anapoyasawiri maisha ya Rosa yaliyojaa taabu na hatimaye kutengana na babake, anaishutumu jamii ambayo imeshindwa kumwelekeza Rosa na vijana wengine kwa kuwapa malezi finyu yaliyo na misingi yake katika ujadi. Mfumo wa malezi katika utamaduni jadi wahitaji kufanyiwa marekebisho fulani ambayo yatawafanya vijana kuwaelewa wazazi wao na hivyo kuishi katika hali ya kutangamana.

Mwandishi anapomtorosha Anastasia kwa mfano, aonyesha kwamba anapinga ndoa ya kulazimishwa - yenye misingi ya

.../35

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

utamaduni wa kijadi. Kitendo hiki chafanana na kile cha mhusika wa J. Kitsao (1980) aitwaye Riziki. Yaelekea waandishi hawa wanawaeleza wazazi kuwa kuwaoza binti zao kwa wazee kwa sababu ya mahari hakuna nafasi katika dunia ya leo. Wasichana wanapaswa kupewa uhuru wa kuchagua wachumba wawapendao. Isitoshe, swala la mahari lisipewe nafasi ya mbele kushinda mapenzi na furaha ya wasichana. Hivyo, jamii ikiendelea kuwalazimisha wasichana kuolewa na wazee basi tuwe tayari kupambana na uasi wa Anastasia, Tumaini na Dennis, jambo ambalo hatima yake ni mikinzano kati ya kambi ya vijana na ile ya wazee.

2:6 Kimalizio:

Katika sura hii tumeona kwamba malezi yaliyo na misingi yake katika utamaduni jadi yamekuwa kiini kikubwa katika kuzua migongano kati ya kizazi kipya na kikongwe. Kupitia wahusika wake Kezilahabi anaelezea maisha na utamaduni wa aina hii ya malezi na athari zake katika maisha ya jamii mpya ya vijana.

Mwandishi anawakumbusha wazazi kwamba dunia imegeuka. Anawahimiza wazazi wakubali kwamba wakati wa kumtunza binti ndani ya nyumba umekwisha. Huu si ulimwengu wa kuambiwa "ulimwengu uko hivi na hivi", bali ni ulimwengu wa kutoka nje, kuona, kuamua na kutenda.

Hili ndilo jambo ambalo wazazi wengi wa jamii za zamani bado hawajalitambua. Ujinga wa aina hii ndio chanzo cha kuangamia kwa vijana wengi wa leo. Hivyo ni maoni ya tasnifu hii kwamba wazazi lazima watambue kuwa pengine maarifa yao ya jana ni ujinga wa leo. Hivyo, hawana budi kuchota kwenye jungu la utamaduni jadi na utamaduni wa leo. yale muhimu na kuyaoanisha ili kuwapa watoto wao

misingi bora yenye mitazamo ifaayo.

Tumeona pia kuwa dini haina nafasi katika kusuluhisha tofauti zilizoko kati ya kizazi kikongwe na kipya. Hii ni kwa sababu dini inaukimbia uhalisi wa mambo kwa kuhubiri maisha bora ya siku sijazo - ahera. Jambo muhimu ni kuweza kusuluhisha matatizo yaliyoko katika jamii mwanajamii atazama katika jamii ili aweze kubainisha kiini cha matatizo yatokeayo.

Hivyo, katika kulishughulikia swala la vizazi, Kezilahabi asema kwamba tutaweza kusuluhisha tofauti kama hizi ikiwa wanajamii ambao ni muungano wa vizazi vingi watatambua kuwa kila kizazi kina dhima yake katika jamii. Kwa mfano, katika jamii nyingi za kiafrika kizazi kipya aghalabu huwa na uwezo wa kuvunja migogoro iletwayo na ukabila na hatimaye kujenga jamii mpya iliyo na misingi yake katika demokrasia halisi. Hivyo, katika muktadha kama huu vizazi vyote vyahitajiana na kutegemeana ili kufaana katika mifumo yote ya maisha. Ili kufikia hatua hii tunahitaji jamii iliyoelimishwa kuhusu shida zinazowakabili wanajamii wake. Katika sura inayofuata tutaangalia athari za elimu ya kimagharibi kwenye jamii na hatima yake.

## 3:0 Sura ya Tatu:

### 3:1 Utangulizi:

Elimu ni maarifa ayapatayo binadamu na ambayo humwezesha kushiriki katika harakati zote za maendeleo ya jamii yake. Kuendelea kwa jamii katika nyanja mbalimbali hasa za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwategemea kiwango cha elimu cha wanajamii wanaohusika. Jamii pia yahitaji kuelimishwa ili ijiauni na idhilali tatu muhimu ambazo ni ujinga, umaskini na ugonjwa.

Elimu ina nafasi muhimu sana katika kuainisha ni nafasi gani wanajamii mbalimbali watakazozichukua katika jamii. Kwa mfano, kupitia kwa elimu tunapata vikundi mbalimbali kama vile cha wazazi na wana wao, ambapo watoto hufikia kiwango cha utu nzima kupitia kwa elimu nyumbani na shuleni.

Mbali na hayo elimu huwa ni chombo muhimu cha kuhifadhi mila na utamaduni wa jamii ili kuweza kuupokeza kwa vizazi vijavyo. Hivyo elimu rasmi inayopatikana shuleni ni jitihada maalum zinazotekelezwa kwa njia maalum zikinuiwa kulitekeleza lile ambalo familia na jamii kwa jumla ilikuwa ikifanya kabla ya jamii kuupoteza ujima wake.

Ingawa madhumuni ya kimsingi ya elimu ni kuleta athari njema zenye kuwaelekeza wanajamii kwa njia bora, kufanikiwa kwake kwategemea jinsi wanajamii watakvyoichukulia. Hii yamaanisha kwamba elimu yaweza pia kuleta athari mbovu na hili ndilo Kezilahabi analoliongelea katika riwaya zake.

Elimu-jamii yasisitiza kwamba ili mtoto aweze kuingizwa na kushiriki kwa kikamilifu katika jamii yake, ni muhimu kupitia katika familia, yaani yenye baba na mama. Hii

yatokana na kule kuaminika kwamba familia humfunza mtoto jinsi ya kukaa katika jamii na jinsi anavyoweza kuitumikia jamii ile ili kuiendeleza, Mckee (1965)[1]. Hivyo baba na mama wameachiwa jukumu la kuwaelimisha watoto wao ili waweze kutekeleza wajibu wao katika uendelezaji wa jamii yao.

Yaelekea Kezilahabi alielewa umuhimu wa familia kuwa msingi wa kwanza katika kuwaelimisha wanajamii. Wahusika wake walio katika kizazi kipya wanapitia hatua hii-jambo ambalo badala ya kuzijenga tabia zao ili waweze kuifaa jamii katika siku za usoni, linaleta mgawanyiko baina ya wazazi na watoto wao. Haya yanajitokeza katika sehemu ya kwanza ya sura ya pili. Tofauti baina ya wazazi na watoto wao zina misingi yake katika sababu kwamba aina ya elimu wanayoipata imeambatanishwa na mfumo wa utamaduni jadi.

Katika sura hii tutajishughulisha na mfumo wa elimu ya Kimagharibi ambayo katika riwaya za Kezilahabi, imemulikwa kama kiini muhimu cha usambazaji wa amali za kisasa kwenye kizazi kipya. Tunataka kuangalia jinsi ilivyochukuliwa na kufahamika na kizazi hiki na uhusiano wake na jamii.

## 3:2 Mfumo wa Elimu ya Kimagharibi

Tumetaja awali kwamba elimu ndicho kiini muhimu katika maendeleo ya jamii. Tutaongeza hapa kuwa ili elimu iweze kuifadi jamii na itekeleze wajibu wake ipasavyo lazima iambatanishwe na mfumo wa kiuchumi katika sehemu hii tunataka kuchunguza ni mambo gani katika elimu ya kimagharibi yasiyoambatana na hali ya maisha ya jamii katika riwaya za Kezilahabi, mambo ambayo hatimaye

1. Mckee, J. (1965): Introduction to Sociology - Uk. 38

yanamtenganisha mwafrika na mazingira yake na hivyo na amali za jamii yake.

Gachukia (1980:115-116) atueleza kwamba wakoloni walipoivamia bara la Afrika elimu ilichukuliwa kama amali iliyothaminiwa sana hivi kwamba familia zilizoweza kuwapeleka watoto wao shuleni zilipata heshima kubwa. Elimu ilichukuliwa kuwa ufunguo wa mafanikio yote ya mtu mweupe. Kupitia kwa elimu wafrika wangeweza kumjua mzungu na hivyo kuweza kukabiliana naye katika nyanja zingine. Elimu pia ilichukuliwa kama chombo cha kuwawezesha kuupata uhuru uliokuwa umechukuliwa na mzungu. Wazazi na wanajamii kwa jumla walitarajia mafanikio mengi kwa kuwaelimisha watoto wao. Hata hivyo sifa kadha za elimu hii ya kikoloni ziliyadidimiza matarajio yao.

Tofauti na ilivyokuwa katika mfumo wa kijadi, elimu ya kikoloni ilidhamiria kuyatumikia maslahi ya kiuchumi ya ulaya. Akilieleza jambo hili Rodney (1972)[2] asema kwamba muundo wa elimu katika jamii za kijadi ulidhamiria kuzisaidia jamii hizo kupambana na mazingira yao. Hivyo, ulitokana na mifumo yao ya kiuchumi na kijamii. Baada ya kuja kwa wakoloni elimu ilelekezwa katika kumfunza mwafrika auhudumie uchumi na kibepari.

Isitoche mwafrika alifunzwa kujisahau na kujiona si chochote si lolote mbele ya mzungu. Hatima yake ilikuwa ni kumkengeusha mwafrika kiasi cha kumfanya ajichukie na kutamani amali zote za uzungu na ubepari. Wazo hili latiliwa nguvu na Ngugi (1972:14) anaposema kwamba:

> Mfumo wa elimu wa kikoloni
> ulimfanya mwafrika amtumikie
> mzungu, ajichukie na kutojiamini.
> Ulidhamiria kuwatenga wafrika
> na jamii yao ... Mfumo huu wa elimu
> uliunda matabaka ambapo mwafrika
> alikuwa katika tabaka la chini.

2. Rodney, W. (1972): <u>How Europe Underdeveloped Africa</u>
Uk. 262

> Ulimteka mwafrika kisaikolojia
> na kumfanya mtumwa wa utamaduni
> wa Ulaya. (tafsri yetu)

Licha ya kumfanya mwafrika mtumwa wa ubepari, ilimzuga hadi kujiona kuwa 'mzungu mweusi'. Kadri mtu alivyopata elimu hiyo ndivyo alivyokengeuka. Jambo hili kama tutakavyoona lilikuwa kiini kikubwa katika kuwatenganisha na jamii zao.

Mbali na kuwateka nyara kiuchumi na kisaikolojia, elimu ya kikoloni pia ilidhamiria kuwatena viongozi wa kisiasa miongoni mwa wasomi hawa ili kuhakikisha kwanba wangechukua hatamu za uongozi baada ya wakoloni kuondoka. Hili ni jambo muhimu kama anavyofafanua Rodney (1972) kwamba jambo hili lilimaanisha kwamba uchumi wa mabepari ungelindwa hata baada ya kuondoka kwao. Jambo hili lilisaidia kudumisha uhusiano kati ya wafrika na mabepari hata baada ya uhuru.

Ni katika muktadha huu ambapo Kezilahabi anachambua viini muhimu vinavyokifanya kizazi kipya (wasomi) kutengana na kile kikongwe.

Akilizungumzia swala la athari za elimu ya kikoloni kwenye kizazi kipya mlacha (1988:49) anaziita athari hizi 'kimbunga' kinachokitisha kizazi kikongwe. Kimbunga hili tunakishuhudia katika <u>Dunia Uwanja wa Fujo</u> (1975) kinapomkabili mamake Leonila lakini kama umeme, kinageuka na kuelekea nyumbani mwake (uk.14). Kimbunga hiki ni ishara ya elimu ya kisasa ambayo ingawa lengo la asili ni 'kukiteka' kizazi kipya kinaishia kuwa tisho la jamii pana. Kama anavyotabiri Mungere kuwa kimbunga kingeitifua mji wake, inakuwa hivyo. Kimbunga hiki tunakiona katika matendo ya Tumaini ambaye baada ya kuvisoma vitabu vingi vilivyohusu mapenzi anafanya urafiki na Leonila jambo ambalo linaishia katika kumpatia mimba. Mimba hii ndiyo inayokuwa kiini cha kugombana kwa Leonila na babake

baadaye.

Katika Rosa Mistika (1971) elimu hii yaonekana kama tisho katika kijiji cha Zakaria Rosa anapopata barua ya mapenzi kutoka kwa Charles. Yeye si mmojawapo wa wanakijiji hicho bali amefika hapo kwa sababu ya elimu. Charles anaweza kuchukuliwa kama athari ya kigeni ambayo yathibitisha kuanzisha kwake dhana mpya za aina ya mapenzi yanayoanza katika umri mdogo sana, na ambayo hayajakubaliwa na mila za kijadi. Kwenda shule pamoja kwa Rosa na Charles kumewafanya marafiki lakini hawangeonyesha hisi zao kwa 'kufungwa' na ujadi. Charles anaamua kumwandikia na kumtumia pesa Rosa anapogudua kwamba wakati waisha na alikuwa karibu kurejea nyumbani. Mapenzi kama haya hayangemstua Zakaria babake Rosa hata kidogo kama yangefuata mkondo wa kitamaduni yaani wa kuwahusisha wazazi na kutolifanya kuwa jambo la siri. Lilikuwa jambo mbaya zaidi kwa sababu Charles alimpatia rosa pesa na akazipokea. Katika hali ya 'kawaida' charles angewatumia wazazi au jamaa zake kutanguliza swala hilo kwa wazaziwe Rosa.

Hata ingawa Zakaria anafaulu kuuvunja uhusiano huu kwa kutumia kipawa cha kitamaduni kama baba, Rosa anaondoka kijijini ili kuendelea na elimu yake katika shule ya bweni. Shuleni Rosa anaingia ulimwengu mwingine ambako wasichana hufanya urafiki na wavulana bila pingamizi zozote; huweka picha na barua zao, hucheza dansi pamoja na isitoche hutembeleana Jumapili. Huu ni ulimwengu wa mashindano ambapo wasichana huwapigania wavulana. Uhusiano huu ambao haungeruhusiwa kijijini unapewa kibali na walimu katika juhudi zao za kujenga umoja kati ya kizazi kipya, umoja ambao una misingi yake kwenye athari za kigeni.

Mamlaka ya masista ni tofauti na ya wazazi. Kuna uhuru wa uhusiano wa kibinafsi kati ya walimu na wanafunzi mradi mwalimu anaweza kumtumia mwanafunzi. Kwa mfano, mwalimu mkuu anampenda Rosa kwa sababu ajua kuwa Rosa ni

.../42

mwadilifu na anaweza kutumika kwa urahisi ili kupata habari kuhusu wengine. Hivyo, kila mwanafunzi anatathminiwa kulingana na malengo ya wale walio mamlakani. Uhuru huu una kiini chake katika suala kuwa, linalomshughulisha mwalimu ni masomo ya kiakademia. Kwa mfano, Rosa anapokosa kushika nafasi ya kwanza ndipo walimu wanapotambua kuwa ameharibika. Badala ya kumsaidia kuirejea tabia na hali yake ya awali, Rosa anaachwa mpaka anapofukuzwa shuleni baada ya kugunduliwa kuwa alikuwa amelala nje ya shule.

Rosa halioni kuwa jambo kubwa kwa kuwa kule kufunuliwa kaida mpya za kijamii na utamaduni mgeni, kunaugeuza mtazamo wake kwa jumla. Amali za kigeni zinawatenga vijana na ujadi wao. Mwalimu Julius Nyerere akilalamika kuhusu amali potovu za elimu ya kikoloni anasema:

> Elimu ya kikoloni katika nchi hii haikuwasilisha amali na maarifa ya jamii ya kitazania kutoka kizazi kimoja hadi kingine; ilikuwa jaribio la kubadilisha maarifa ya kijadi kwa yale ya jamii tofauti.[3]

Mbali na amali za kigeni elimu ya kikoloni ilimtenganisha mwafrika na utamaduni wake kwani lile tendo la kumpeleka mtoto shuleni mbali na nyumbani lilikuwa ni kama kumpatia uhuru wa kujiamulia masiala yote katika maisha yake jambo ambalo halikuweko katika mila na tamaduni za kijadi.

Hali hii inazua hisi na vitendo vipotovu katika jamii ya kizazi kipya. Regina mamake Rosa anailaumu elimu kwa kuwafanya wasichana watoe mimba ili waweze kuendelea na masomo (uk. 18). Mabadiliko haya yanatukia ghafla mno hivi kwamba hakuna kizazi kinachoweza kuyakabili ilivyo.

3. Nyerere, J. (1968): Education for Self Reliance Uk. 47

Hatima yake inakuwa ni kuzua mgongano kati ya kizazi kikongwe na kile kipya.

Katika Kichwamaji (1974) athari za elimu zinaingia kijijini kwa nguvu kutoka mjini. Kazimoto ambaye ni mwanafunzi wa chuo kikuu anataka kulipiza kisasi kwa sababu dadake ametungwa mimba na Manase rafikiye. Kazimoto anapoenda nyumbani wakati wa likizo, ana mawazo ya kufanya chochote kitakachomuudhi Manase. Anafanya mapenzi na dadake Manase na pia Vumilia rafikiye Manase. Kwa kuwa amepitia chuoni, jinsi uhusiano wa kimapenzi kati ya msichana na mvulana unavyoeleweka umegeuka. Tofauti na ule wa jadi kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya mvulana na msichana. Kazimoto kama Tumaini wa Dunia Uwanja wa Fujo ameamua kuwachezea wasichana bila kujali matokeo yake. Wazazi hawaelewi uhusiano huu. Kwa mfano babake kazimoto anamlaumu mwanawe (Kazimoto) kuwa ameyasahau mambo ya nyumbani kwa sababu ya wasichana. Kazimoto anapokana babake anakasirika na kumkanya kuwa asimdanganye tena. Tegemea pia mamake Vumilia anagombana naye kwa sababu ya 'kutembea' na bintiye (uk.105-106).Isitoche mamake mwenyewe Kazimoto aonekana mwenye masikitiko mengi kwa yale yaliyomfika mwanawe Rukia. Kama mamake Rosa wa Rosa Mistika (1971) anaulaumu msiba uliomfika Rukia kwenye matendo ya vijana wa leo ambao mbali na kukengeushwa na elimu ya kikoloni waelekea wamejichukulia sheria mikononi mwao.

Manase ambaye ndiye aliyesababisha msiba huu anaandika barua kwa wazazi wake. Kama alivyofanya Tumaini wa Dunia Uwanja wa Fujo, anadai kuwa hawezi kumwoa Rukia kwa sababu amepata mchumba mwingine. hata bila ya kuwaarifu wazaziwe anaamua kumwoa Salima, kabla kama anavyosema. hawajamfanyizia matata zaidi. (uk. 132). Kabengo babake Manase analemewa, hajui afanye nini. Twaonelea kwamba mwandishi anailaumu elimu iliyokosa kuwafundisha vijana maadili bora, kwa kuleta uhusiano usiofaa kati ya wazazi na watoto wao. Manase ameyavunja maadili ya kijamii kwa kufanya mapenzi na Rukia, ambaye

kulingana na maadili ya jamii apaswa kuchukuliwa kama dadake.

Kutokana na haya yaonekana kwamba ukweli wa mambo kuhusu swala la kuwapeleka watoto shule haukufahamikiwa wazazi mpaka mikinzano ilipoanza kutokea. Mikinzano hii inatokea kwa sababu ya kubadilika kwa uhusiano baina ya watoto na wazazi wao ambapo wazazi wanatamani kuhifadhi uongozi na mamlaka yao ya kijadi na wakati huo huo ukiwa umechukuliwa na mwalimu wa kimishenari.

Kazimoto anafanya mapenzi na rafikize 'machoni' mwa kakake Kalia ambaye kwa kutojua kwake anamwiga kakake mkubwa tendo ambalo linasababisha mgongano mkubwa kati yake na wazee wa kijiji chake kwa kuwanajisi wanawake. Hali hii imekithiri hadi anapewa jina la 'nunda mla watu'. Kilele chake kinafikia anapokamatwa na watu na kutozwa faini, kitendo ambacho kinamgadhabisha babake hadi anapoamua kumfukuza nyumbani. Maneno yake yanatukumbusha yale ya Zakaria alipomkana Rosa bintiye; Anamwambia Kalia:

> ...Sitaki kukuona tena mjini
> kwangu. Na hata nikifa usije
> kulia mbele ya kaburi langu (uk. 124)

Mgongano huu unatukia kwa sababu kizazi kipya kimeziingilia amali za kigeni kwa pupa jambo ambalo limetokana na aina ya elimu wanayopata shuleni. Mabadiliko ya mamlaka pia yametokana na elimu ya kisasa. Watoto wametolewa mamlakani mwa wazazi wao na jamii ya kijadi na kuwekwa mikononi mwa walimu na jamii ya kimagharibi. Hii yamaanisha kwamba mtu anatenganishwa na jumuiya yake na kuwekwa katika jamii iliyoundwa na watu wa jamii tofauti. Chini ya mamlaka ya walimu wanaochukua nafasi ya wazazi kunaibuka aina mpya ya jamii inayapingana na ile ya jadi. Kutenganishwa huku kunasaidia kuujenga msingi thabiti wa jamii mpya. Katika hali ya kuelimishwa na kuelezwa kuhusu ulimwengu wa nje na

.../45

ambao ni tofauti na mila zao kizazi kipya chajipata katika hali mpya kama inavyojitokeza katika riwaya ya Gamba la Nyoka (1979). Kutokana na elimu aliyoipata shuleni Tinda anaupata ujasiri wa kuweza kukabiliana na mamake na kumuuliza maswali ambayo hangeuliza katika hali ya ujadi. Mwandishi atueleza kuwa:

> Tinda alikwenda Jikoni kwa furaha. Moyo wake ulikuwa umetulia. Alikuwa amethubuti kumwambia mamake mambo yaliyokuwa yakiusumbua moyo wake kwa muda mrefu (uk. 11).
>
> (msisitizo ni wetu).

Umbali unaoumbwa kati ya wazazi na watoto wao ni mpana hivi kwamba hawawezi kuhisi mamlaka ya wazazi au hata utamaduni wa jadi juu yao. Rosa katika Rosa Mistika (1971) anachanganyishiwa na fikra anapodhihirikiwa kuwa kuna tofauti ya umbali kati yake na babake na hivyo hawezi kujua anachokitenda. Ni uhuru huu kutoka kwa mamlaka ya jadi unaomfariji na kumpa nguvu ya kuweza kuamua kuungana na wasichana wengine katika ukumbi wa dansi.

Katika kiwango kingine elimu inawapofusha vijana hadi kufikia kiwango cha kutowajali wazee wao na hatimaye kutoijali jamii yao pana. Katika Gamba la Nyoka (1979) mamboleo na mambosasa ni wawakilishi wa kizazi kipya cha vijana waliosoma na wenye madaraka. Wanawahamisha wazee bila kuwaeleza maana ya vijiji vya ujamaa. Ujumbe wanaouleta vijijini unawaletea wazee huzuni nyingi. Mwandishi atueleza hivi kuhusu mama Tinda:

> Hakuweza kumalizia. Machozi yalianza kumlengalenga. Hiyo 'kesho' ilitia huzuni kubwa moyoni mwake (uk.12)

Ujumbe wao unawahamakisha wanakijiji wa Bucho ambao

wanaamua kukataa kuhama na hivyo kupigana na wanamapinduzi hawa, ambao kulingana na wazee wa kijiji ni watoto wao wenyewe ambao wamechukua mamlaka ya uongozi kutokana na elimu waliopata (uk.15-16). Hivyo, kwa kuwa 'sikio halina nguvu mbele ya kichwa' wanaamua kukataa mwito wa kuhamia mjini - uamuzi huu unazusha mgogoro kati ya wanakijiji na watawala jambo ambalo linaishia katika vita ambavyo hatima yake ni vifo. Vita hivi basi vyapaswa vichukuliwe kama tokeo la mgongano kati ya kizazi kikongwe na kile kipya cha vijana waliosoma.

Kisa kama hiki pia tunakipata katika <u>Kichwamaji</u> (1974). Hapa tunakutana na Manase aliyehitimu shahada ya chuo Kikuu na kupta kazi kama mkuu wa wilaya. Hata hivyo yeye haihudumii jamii yake ipasavyo. Anaupoteza muda kwa kucheza na wasichana marafikize. Mzee anapoingia ofisini mwake anamfukuza - kisa na maana, ameingia na fimbo! Mwandishi atueleza kwamba:

> Mzee alipotolewa nje alikuwa kama mtu mwenye wazimu. Alikuwa akitetemeka kwa woga .... Mzee alipokuwa akitoka nje sikuona kitu kingine isipokuwa kwamba wazee walikuwa wakitukimbia. <u>Uhusiano kati yao nasi ulikuwa ukikatika</u>. Niliona wazazi waki-wakimbia watoto wao ambao sasa walikuwa kama simba ... (uk. 7)
> (msisitizo ni wetu)

Kisa hiki ni mfano mzuri wa farka iliyoko kati ya Kizazi kipya (cha wasomi) na kile kikongwe. Hii yamaanisha kuwa hakuna uhusiano wa maana unaoweza kujengwa kati yao. Hatima yake ni kushindwa kwa wasomi wenye madaraka kuyatekeleza ipasavyo jambo ambalo lawafanya kuwadhuhumu

wazee.

Elimu yenye misingi ya kigeni kinachopata kizazi kipya inaonekana kama kiini kikubwa kinachowatenganisha na kizazi kikongwe. Akilishadidia jambo hili mwandishi anasema:

> Nilipofika kitandani niliona kwamba mazungumzo tuliyokuwa nayo yalionyesha tofauti kubwa iliyokuwapo kati ya wazee wetu na sisi. Kweli wazee wetu tulikuwa tumewaacha mbali. Kati yetu na wazee kulikuwa na sehemu kubwa sana ambayo ilihitaji kujazwa (uk.145).

Mfumo wa elimu wa kimagharibi waonekana kuyatekeleza mahitaji ya kibinafsi jambo ambalo laonekana ni tofauti na mfumo katika elimu ya kijadi ambayo ilisisitiza mahusianao na tabia mwafaka kwa wote. Hivyo ukweli wa mambo ni kwamba pale ambapo mfumo mmoja hutilia mkazo uhusiano mwafaka kijamii, mwingine huegemea kwenye maslahi ya kibinafsi.

Katika sehemu hii tumeona jinsi mielekeo tofauti ya vizazi hivi viwili unavyoathiri uhusiano kati ya kizazi kipya na kile kikongwe. Elimu ya kigeni ndiyo inayowapa vijana uwezo wa kushindana na wazee wao.

### 3:3 Ujumbe wa Mwandishi:

Kama tulivyotangulia kusema, ni kwamba hata ingawa madhumuni ya kimsingi ya elimu ni kuleta ufanisi katika jamii, haiwi hivyo kila mara. Elimu pia imekuwa chanzo cha uharibifu wa jamii na hili ndilo Kezilahabi alilonuia kulionyesha katika riwaya zake.

Senkoro (1976:88) amedai kuwa mkabala wa jamii umekuwa kwamba mtu huwa wa maana akiwa na cheo cha juu tu, yaani akiwa na elimu. Maelezo juu ya matilda kwa mfano yanaoyesha jambo hili:

> ...Matilda alikuwa mwanamke
> mzuri sana. Ingawa alikomea,
> darasa la saba watu wengi wa
> maana - yaani wenye vyeo
> vya juu walipeleka posa (uk.55)
> (msisitizo ni wetu).

Hali na imani hii imeleta mgongano mkubwa na kuasilisha upotovu kama ule tuliouona kati ya Manase na mzee au vijana wanamapinduzi, Mambosasa na Mamboleo wa Gamba la Nyoka (1979).

Natharia ya uyakilifu wa Kisoshiolisti inasisitiza kuwa mabadiliko hayana budi kufanywa pale inapolitajika. Hivyo mwandishi aelekea kupendekeza kufanywe mapinduzi pande zote zinazosababisha mambo hayo. Yatupasa basi tuuibadili vyombo vyote kama vile elimu vinavyoathiri wanajamii na kuleta mgongano wa aina hiyo.

Katika tamthilia ya <u>Wakati Ukuta</u> (1971) ya E. Hussein kwa mfano, mwandishi anajaribu kutoa suhuhisho baada ya kutambua kuwa mambo kama vile elimu, magazeti ya tamaduni za kigeni, filamu na mengineyo yasababisha mgongano huu wa vizazi. Baba Tatu anakiri kuwa:

> Tatu amesoma vitabu vya
> kizungu, ameona mtoto wa
> kike na wa kiume wanatembea,
> wanakwenda sinema au dansini ...[4]

Anaona kuwa ili kuitatua migogoro hiyo, lazima watu wajirekebishe. Lakini swali ni kwamba watajirekebisha vipi? Anaendelea kueleza:

... tukaze, lakini tikiona
kamba karibu kukatika, tulageze...[5]

Jambo ambalo Hussein haonyeshi kwa wazi ni vipi tukaze na tulegeze kamba katika maisha halisi.

Hivyo ni maoni ya tasnifu hii kwamba kama mwafrika atapata faida yoyote kutoka kwa elimu ya kimagharibi, mafunzo yapaswa yaelekezwe katika kuimarisha mahusiano ya kimsingi ambayo ndiyo misingi ya maadili na uundaji wa hulka. Madhumuni ya elimu hupatikana kutokana na hamu ya kufanikiwa katika kupata maarifa ya ujuzi unaohitajika. Lakini tukumbuke kuwa maarifa na ujuzi ni swala la kando sio lengo muhimu katika mfanyiko* huu.

Maarifa anayopata mtu lazima yaende sambamba na harakati za kila siku hasa za kiuchumi, kikazi na kijamii. Tabia pia lazima itiliwe mkazo iwapo harakati za jamii kwa jumla zitaimarishwa. Jambo hili litaweza kuziba tofauti zilizopo kati ya wanajamii na hivyo kuwa na msingi bora wa maendeleo.

## 3:4 Kimalizio

Katika sura hii tumeonyesha jinsi elimu inavyotumika kama chombo cha kuvitenganisha vizazi katika jamii. Elimu inamulikwa kama chanzo kikubwa cha makundi mawili yaani la wasomi (vijana na watawala) na la wasiosoma (wazee na watawaliwa). Kupitia riwaya hizi nne, Kezilahabi aonyesha vile ambavyo elimu inakuwa chombo cha kugawanya katika jamii, badala ya kuiendeleza.

Mwandishi anaimulika elimu ya kikoloni kama chanzo cha baadhi ya matatizo yanayoikumba jamii. Hii ni kwa sababu badala ya kuistawisha jamii, elimu yaonekana kama kiini

.../50

cha maovu badala ya mema. Kezilahabi haoni matumaini yoyote katika elimu ya aina hii.

Katika sura inayofuata tutaangalia jinsi uchumi na taratibu za maisha ya jamii zinavyokuwa kiini cha mikinzano kati ya wanajamii.

4 & 5 Katika Senkoro (1976): 'Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili' Uk. 89

* Msamiati huu umetumika hapa kwa maana ya neno la kiingereza "process". Tafsiri hii ni kwa mujibu wa Kamusi ya Isimu.

## 4:0 SURA YA NNE:

### 4:1 Uchumi na Jamii:

Utamaduni wa jamii yoyote ile ni mfumo wa maisha kwa jumla na hivyo hatuwezi kutenganisha uchumi wa jamii na fani zingine za maisha. Fasihi ina wajibu wa kuonyesha uhusiano huu na kudhihirisha kwamba wakati uliopo una misingi yake katika wakati uliopita na wakati ujao unazalika katika wakati uliopo.

Riwaya nyingi za Kiswahili zonyesha waziwazi kuwa utamaduni hutokana na uhusiano baina ya uchumi na taratibu za maisha ya jamii nzima.[1] Ikiwa kwa mfano, uchumi mpya utaleta taratibu mpya za maisha, basi hapo hapo ama utatokea mwingiliano wa taratibu mpya na zile za zamani au mgongano kati ya taratibu hizo za aina mbili kama tutakavyoona katika riwaya za Kezilahabi.

Tasnifu hii inayashughulikia mahusiano ya wanajamii hivyo ili kuyaainisha katika ukamilifu wake inakuwa ni muhimu kuyahusisha na masiala ya kiuchumi kwani wanajamii wale wale ndio wanaohusika katika nyanja za kisiasa, Kielimu, Kiuchumi na Kidini.

Mfumo wa uchumi katika jamii ni msingi muhimu wa kuainisha uhusiano wa watu katika jamii hiyo na pia uhusiano na harakati za kitabaka pale ambapo pana matabaka. Lakini pia hatuna budi kukiri kuwa:

> ...Mahali popote pale ambapo
> ukoloni ulitokea, kuletwa kwa
> mambo ya uchumi kuliandamana
> sana na pesa... kumeleta

1. Senkoro, F.E.M.K. (1976): Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili. Jarida la T.U.K.I. Uk. 86

> kupondekapondeka kwa mambo ya kimila ... kuteguka kwa jamii nzima kiutamaduni na kiuchumi na pia kuanguka kwa umoja wa jamaa ....[2]

Katika sura hii tunataka kuangalia jinsi swala la uhusiano baina ya uchumi na jamii lilivyokabiliwa na Kezilahabi na ni kwa kiwango gani madai kama haya ya Aime Cezaire yanaweza kuchukuliwa kama yenye uhalisi wa maisha.

Watson (1956) amedai kuwa njia maalum ambayo wakulima na wanajamii asilia wanaweza kuhusika katika uchumi wa kilimwengu, ni kwa kujiunga na mfumo wa uajiri kazi kwa malipo, au kwa utengenezaji bidhaa zinazoweza kuuzwa katika soko la kimataifa. Kujiunga na mfumo wa uajiri kazi kwa malipo mara nyingi huwa kiini kimojawapo cha mikinzano kati ya vizazi na huibua matatizo yanayohusu usimamizi wa mapato. Jambo hili aghalabu huufanya muundo wa kijamii kuporomoka.

Uhusiano huu wa kijamii unaotokana na njia au zana tofauti za kiuchumi umemulikwa katika katika riwaya za Kezilahabi. Hivyo tunadhamiria kuangalia ni kwa njia gani taratibu mbalimbali za kiuchumi katika jamii inayomulikwa na mwandishi zimekuwa sababu ya kuvitenganisha vizazi yaani kipya na kile kikongwe.

## 4:2 <u>Uchumi katika Ujadi:</u>

Kwa kuwa malengo yanayonuiwa kufikiwa katika medani ya kiuchumi yapaswa kwenda sambamba na madhumuni ya nyanja

2. Makala ya Aime Cezaire: 'Culture and Colonzation' Katika Senkoro (1976): Uk. 83.

zingine katika jamii, hatuna budi kuigusia nyanja hii ili kuona vipi iliathiri uhusiano wa wanajamii katika jamii ya Kezilahabi. harakati zote za kiuchumi zitakuwa na maana kama zitahusishwa na desturi za jamii inayohusika.

kabla ya mapinduzi ya viwanda uchumi na nyenzo zake ulitegemea ukulima katika jamii nyingi za kiafrika.[3] Katika kila familia yaani, baba, mama na wana walikuwa ni sehemu moja ya kiuchumi. Jambo hili lilitiliwa nguvu na mgawanyiko wa kazi kulingana na uana. Kila mmoja katika familia alijua na kuielewa nafasi na kazi yake aliyotarajiwa na jamii aitekeleze katika juhudi zake za kuzalisha uchumi na kugawanya riziki za familia ili kuhakikisha ukuzaji wa mali wa kundi hilo.

Makabila mengi nchini Tanzania yaliendesha uchumi wake kwa njia ya ukulima wa mashamba madogo madogo ya chakula, usasi na ufugaji.[4] Kabila kama la wangoni kwa mfano, liliishi kwa kushambulia makabila mengine ili kupata mifugo. Muhimu zaidi ni kuwa ardhi ilikuwa ni mali ya wote. Jambo, hili lilihakikisha kuwa kila mwanajamii alikuwa na mahali pa kulima na kuishi. Jambo hili ndilo linalomfanya babake Kazimoto kupewa na serikali baadhi ya mashamba ya Kabenga kwani Kabenga hakuwa akiyatumia yote.[5] Jambo hili latufahamisha kwamba kila mwanajamii aliweza kupata mahala pa kuishi na kulima ili kujipatia riziki.

Kazi kama harakati nyinge yoyote ya kijamii ilitekelezwa kulingana na desturi za jamii. Hii ilihakikisha kwamba kila mtu aliitekeleza kwa njia mwafaka kazi yake aliyotarajiwa na jamii bila kusababisha mikinzano yoyote. Ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku walichukuliwa kama sehemu muhimu ya utajiri wa jamii mbali na kuwa asili mojawapo ya riziki yao. Jambo hili twaliona katika zile familia za kijadi katika

3. Kenyatta, J. (1961): <u>Facing Mount Kenya.</u> Mercury Books, London. Uk.312
4. Iliffe, J. (1971): <u>Agriculture change in Modern Tanganyika.</u> Uk. 8
5. Kezilahabi (1974): <u>Kichwamaji</u> - Uk. 111

jamii ya kezilahabi. Katika Rosa Mistika kwa mfano, Zakaria na Regina wanamuuza ng'ombe ili wapate pesa za kumpeleka Rosa shule ya upili.[6] Huu ndio uliokuwa utajiri wa jamii.

katika Kichwamaji mwandishi anatuchorea maisha ya wanakijiji wa ziwani ambao ni wavuvi. Yaelekea walifanya kazi ya uvuvi kwa kushirikiana kama anavyotudokezea mwandishi:

> Nilipofika Ziwani nilikuta
> wavuvi watano wakishona
> matundu ya mitego yao.
> Walikuwa wakifanya kazi
> hii kwa haraka sana. Mikono
> yao ilikuwa mvepesi sana.
> Walikuwa wakifanya kazi
> hii hali wakisimuliana hadithi.[7]

Mbali na uvuvi jamii ya Kezilahabi pia iliendesha uchumi wake kwa uwindaji. Katika Gamba la Nyoka tunafahamishwa na mwandishi kuwa mumewe mama Tinda aliyepewa jina la majazi, 'Bwana Nyama', alikuwa mwindaji hodari. Alifariki siku moja alipoitwa kwenda kuua viboko waliokuwa wakiharibu mazao ya watu.

Vijana waliungana na wazazi wao katika ukuzaji na ugawanyaji wa riziki za familia na utajiri wake hadi wakati wa ndoa. Kwa mfano katika Dunia Uwanja Wa Fujo Misana, mtoto wa kasala na Mungere ndiye aliyepewa jukumu la kuwachunga ng'ombe ilhali wazazi wake walifanya kazi ya kulima shambani. Ugawanyaji huu wa kazi ulihakikisha kwamba kila mwanajamii alikuwa na nafasi yake muhimu katika kuhakikisha kuendelea kwa jamii katika nyanja ya uchumi.

Ubadilishanaji wa bidhaa ulikuwa ni aina mojawapo ya biashara ilivyokuwepo lakini haikuwa ni kwa madhumuni ya

6. Rosa Mistika - Uk. 15

7. Kichwamaji - Uk. 49

kujipatia faida. Mazao yaliweza kubadilishwa kwa mifugo kama vile mbuzi au ng'ombe.[8]

Mabadiliko mengi katika maisha ya kiuchumi ya wakulima na jamii asilia yametokana na kupanuka na usambasaji wa miundo ya kimagharibi ya harakati za uchumi. Jambo hili limetokana na kuanzishwa kwa viwanda na utaratibu wa biashara katika jamii hizi asilia za wakulima. Kutukia kwake kumekuwa kiini mojawapo kinacholeta mgawanyiko wa wanajamii kama tutakavyoona katika sehemu inayofuata.

## 4:3 Athari za Kiuchumi-jamii:

Kuzuka kwa miji, mambo ya viwanda na uchumi ulioambatana sana na mambo ya pesa kumegawanya jamii kukawa na wale wanaoishi mijini wakifanya kazi na pia wale wanaobaki vijijini, wakulima. Maisha ya mijini yanaonyesha tofauti kubwa sana na yale ya vijijini. Haya yana utamaduni wake tofauti na ule wa vijijini ambao kwa kiasi kikubwa una athari za kikoloni. Jambo hili ndilo linalosababisha tofauti baina ya kizazi kikongwe ambacho aghalabu ndicho kinachobaki vijijini, na kile kipya ambacho huingilia maisha ya mijini.

Katika Dunia Uwanja wa Fujo Kezilahabi analishughulikia swala la mvutano wa nguvu za kiuchumi ambazo zaonekana kuyaainisha matendo ya mtu na mtazamo wake kuhusu maisha. Kwa mfano Tumaini ana nguvu za kuwalaghai wasichana, kuwatia mimba na kuwasahau kutokana na nguvu za kiuchumi alizo nazo. Tumaini ni kijana aliye na pesa ambazo katika jamii ya Tanzania hasa kabla ya Azimio la Arusha zilionekana kuwa ni msingi wa maendeleo yote. Hivyo, anajitenga na wanajamii wengine jambo ambalo limetokana na kujihisi kuwa tofauti na mwenye mamlaka kwa wanakijiji. Kutokana na vitendo vyake viovu, anawahamazisha wazee wa kijiji kiasi cha kumtaka ahame kijijini.[9]

8. Iliffe, J. (1971): Agriculture change in Modern Tanganyika - Uk. 8
9. Dunia Uwanja wa Fujo - Uk. 39

Akilizungumzia swala la mivutano ya kiuchumi analoliita swala la vinvume (antithesis), Senkoro (1992:82) anaonyesha jinsi tofauti za kitamaduni kati ya maisha ya vijijini na vale ya mijini yanavyomulikwa na Kezilahabi. Tunauona mfumo wa kijiji ambao umo katika hatua za kubomoka kwani msingi wa mfumo wa uchumi wake unapotea kwa kupigwa kumbo na msingi wa uchumi wa kibepari. Kutokana na ukweli huu wa kihistoria tunaona katika Dunia Uwanja wa Fujo athari za maisha ya mijini juu ya yale ya kijijini. Kwa mfano, utulivu wa kawaida wa kijijini tunauona unavvoingiliwa na "fujo" za mijini za akina Makoraboi na Tumaini ambao wametawaliwa sana na utamaduni wa kifedha ambao aghalabu huyatawala maisha ya mijini. Maisha ya watu kama hawa yameyaingilia yale ya vijijini na kusababisha utengano baina ya wanakijiji.

Mji umeambatana sana na imani kubwa walio nayo watu juu ya pesa. Mfumo wa mji unazaa watu wenye pesa waishio maisha ya anasa na starehe, wakati ambapo mji huo huo una maskini hohehahe, malofa wasio na kazi. Hii ndiyo sababu mwandishi kama Ohly (1981:36)[10] anaonelea kwamba miji ina maovu mengi ya kijamii ambayo yanweza kuyaharibu maisha ya vijana.

Katika Rosa Mistika tunaona mfano mzuri wa maisha ya mji. Ulevi na umalaya ni picha mojawapo ya maisha kama haya:-

> ...Hapo alikaa akinywa chupa yake ya kilimanjaro kwa raha. karibu na meza yake walikuwa wamekaa vijana wawili. Mmoja alikuwa amekwishalewa sana. Alikuwa ameweka kichwa chake juu ya meza ... Mwanamke mmoja kijana mfanyakazi wa huko alikuwa amekaa juu ya magoti yake, alikuwa akimpapasa kiuno na

10. Olly, R. (1981) - Aggressive Prose, Dar es Salaam Uk. 36

> maziwa - ... kuzunguka meza hiyo hiyo tu kulikuwa na wanawake wengine sita ... chupa zilikuwa zimejaa hapo. Martin na Cinzano pia zilikuwepo. Baada ya muda kitambo, yule kijana alimwamsha mwenzake ili waende ... Rosa alisikia vijana hao wakisema: "lakini, msitundanganye! Kesho tutakuja kuwachukua". "Sisi ni mali yenu tu! Walijibu kwa pamoja, msemo wao wa kawaida.[11]

Mbali na uovu wa maisha ya ulevi na umalaya, kuna pia ujanja na unafiki. Yaelekea mwandishi atueleza kuwa hali hii imetokana na athari za kiuchumi kwenye kundi hili la wanajamii. Vijana kama Rosa bila shaka wanaishia kuathirika na maisha kama haya. Tunaelezwa kuwa:

> Baada ya kisa hiki kijana mmoja alikwenda kukaa meza moja na Rosa. "Unatumia nini dada yangu?" "Tusker,". Tusker moja iliagizwa kwa ajili yake. Rosa alikunywa chupa tatu. Alimwambia kijana aje kumchukua kesho yake namba mbili "Banda Street"... Rosa alifahamu siku yake ya kuondoka kwenda Morogoro. Kesho yake aliondoka. Rosa alifahamu mengi ... alifahamu mapenzi ya unyonyaji. Yule kijana alifika "Banda Street" namba mbili. <u>Hata kiwiliwili chake kilimcheka.</u> (uk. 52-53)
>
> (msisitizo ni wetu.)

11. <u>Rosa Mistika</u> - Uk. 52

Haya ndiyo matokeo ya maisha ya mjini. Wazee wenye pesa na mamlaka ni baadhi ya watu wengine wanoingiliana na wasichana kama kina Rosa. Wazee hawa wanatumia uwezo wao wa kifedha kuwapata wasichana maskini kama Rosa. Jambo hili linawafanya wasichana kuwa mawindo rahisi kwa watu wenye tabia mbaya. Hili twalishuhudia Rosa anapocheza dansi na Deogratias, mzee wa miaka arobaini aliye na wake wawili.

Wazee wengine wanaohusiana na Rosa ni kama vile mkuu wa chuo cha ualimu cha Morogoro na mkuu wa wilaya anayefika kumpeleka Rosa 'Beach' waka-pumzike. Hawa ndio wanaompa Rosa uhuru wa kufanya atakavyo. Ingawa kwa mujibu wa vyeo vyao wanatakiwa kuwalea vijana kama Rosa, wanafanya kinyume cha matarajio ya jamii. Hali hii inazusha hisi za uasi katika vijana na hatima yake inakuwa kwamba vijana hawaoni ni kwa nini wawaheshimu wazazi wao. Tunamwona Rosa akimtusi babake mbele ya mkuu wa wilaya (uk. 70). Kitendo kama hiki kinazorotesha uhusiano baina ya vijana na wazazi wao.

Mbali na kuwa mahali penye uovu mwingi miji imechorwa na mwandishi kama mahali penye ukosefu wa maadili. Jambo hili twalishuhudia katika riwaya ya <u>Kichwamaji</u> (1974). Kwa mfano, Manase ambaye amepewa cheo cha mkuu wa Wilaya anamnajisi Rukia dadake Kazimoto na kumtunga mimba. Ukosefu huu wa maadili waweza kuwa na chanzo chake katika hali anayoieleza Musau (1985:81) kwamba, watu wanapotoka vijijini na kuingia mijini kufanya kazi, huwa wameziacha koo zao na makabila yao vijijini. Wafikapo mijini hujiona kuwa watu huru kutokana na sheria na kaida za watu wao. Hivyo huwa rahisi kwao kujiingiza katika maovu kwani mila za koo na makabila yao, huwa hazipo kuyaongoza maisha yao. Hata hivyo la muhimu zaidi ni kwamba uchumi wa miji unaothamini pesa sana huwa hauna budi kubadilisha tabia zao.

Yaonekana mwandishi atwambia kwamba pindi watu watokapo vijijini ambako maisha yanatawaliwa na kanuni

za koo na makabila yao, na kuingia mjini kutafuta kazi tabia zao hubadilika na aghalabu huwa mbaya. Jambo hili lina chanzo chake katika mfumo mpya wa kiuchumi ambao huwa ni Kishawishi kikubwa cha vijana, chambilecho Jomo Kenyatta (1961:314) kuwa tatizo la maadili latokana na mfumo wa uchumi wa kijamii.

Vumilia bintiye Tegemea, kwa mfano, ni kijana anayejiingiza katika umalaya katika juhudi zake za kutafuta riziki. Jambo hili ndilo linalomtia mikononi mwa watu katili wanaomnajisi wakidai kwamba amekula pesa zao. Hiki ni kitendo cha watu waliokosa utu, jambo ambalo latokana na mfumo wa uchumi wa mji unaotawaliwa na pesa, ambapo pesa zaonekana kuthaminiwa zaidi ya kitu kingine kile. Hatima yake ni kwamba uhusiano wa watu katika miji unaonekana kutawaliwa zaidi na pesa kuliko utu. Maisha ya aina hii yanapingana vikali na aina ya maisha ya kijijini ambapo mtu anakulia na kulindwa na utamaduni wa jadi.

Kupitia kwa familia ya Vumilia na Moyokonde; na ile ya Manase na Pili, twashuhudia kuweko kwa tabaka za kiuchumi katika miji. Maisha wanayoishi Moyokonde na Vumilia ni ya kimaskini sana. Uhalisi wa jambo hili waweza kuonyeshwa kupitia kwa maelezo kuhusu nyumba wanamoishi:

> Nyumba hii ilikuwa na vyumba viwili: cha kulala na cha maogezi. Paa lilikuwa karibu, vile kwamba nilikaribia kuligusa kwa kichwa. Madebe yalikuwa na matundu mengi na nilishangaa kama kweli waliweza kulala humo wakati wa mvua. katika chumba cha maongezi niliona viti viwili vya kuegemea, mtungi wa maji na kabati ndogo...[15]

15. Kichwamaji - Uk. 183



UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Umaskini huu ni kinyume cha utajiri wa kina Manase ambao wanaishi katika jumba kubwa, wana gari, radiogramu n.k.

Tofauti hizi za kiuchumi ndizo zinazowafanya vijana kama Vumilia kuwa mawindo rahisi kwa wanaume. Kutokana na masumbuko mengi ya maisha katika jitihada zao za kutafuta riziki wanaishia mikononi mwa watu kama Moyokonde. Isitoche, yanawapa vijana "ushujaa" wa kuyakabili, ambao hatima yake ni migongano kati yao na wazazi wao. Jambo hili lajitokeza wazi Vumilia anapokataa kurudi nyumbani na mamake Tegemea. Anakiri kwamba:

> Maisha yangu magumu lakini
> nayaona mazuri. Nami sasa
> nina bwana. Siwezi kumtupa.
> Tuliokotana maskini na tuta-
> tunzana mpaka tutakapokufa na
> umaskini wetu. Siwezi kumwacha
> bwana'angu. Uk. 184[16]

"Ushujaa" huu ndio unaomfanya Vumilia kumwambia mamake kwa ujeuri mwingi kwamba:

> Mimi sitaki maneno mengi...
> ninataka kukuuliza swali moja
> ambalo ulikataa kunijibu tangu
> zamani: Je, baba ni nani?
> ... Basi fahamu kwamba maisha
> yangu yalianzia hapo kuharibika;
> kutofahamu nani baba yangu. UK. 185 [17]

Kumlaumu mamake kwa hali yake duni kiuchumi labda kwatokana na ukweli wa mambo kuwa, kubadilika kwa jamii asilia na kuwa jamii yenye ustaarabu, kulianzisha mfumo

16. Kichwamaji - Uk. 184

17. Kichwamaji - Uk. 11

wa urithi upande wa baba. Jambo hili lilimaanisha kwamba waliotawala kiuchumi walikuwa wale waliomiliki nyenzo na njia zote za uchumi, nao walikuwa ni wanaume. Hivyo, kama Vumilia angalikuwa na baba basi labda hangejiingiza katika maisha potovu ya mjini akitafuta riziki.

Hali kama hii ndiyo inayotukia katika Gamba la Nyoka. Anapofiwa na bwanake, mama Tinda hapati msaada wowote kutoka kwa jamii ili kuyaendesha maisha yake na watoto wake. Hatimaye mahitaji ya pesa yanamsukuma kuwa hawara wa padri Madevu. Mama Tinda anauona uhusiano wake na Padri kama baraka kwa jinsi anavyomkidhia haja zake za kiuchumi. Ndiposa anapohamishwa katika kijiji cha ujamaa, anajengewa nyumba nzuri ya bati. Uhusiano huu unamchukiza Tinda mwanawe ambaye anakiri kwamba:

> ...Mama, mimi Padri Madevu
> simpendi! Uk. 11 [18]

Matamshi haya vanamkasirisha mamake ambaye amamwonya na kumtahadharisha kwamba kama si yeye hawangepata pesa za kujikimu. Hivyo, tofauti kati ya mama na mwana hapa zina msingi wake katika suala la uchumi. Tinda aelekea kutokubaliana na mamake kuhusu jinsi wanavyopata fedha.

## 4:4 Kimalizio:

Jambo linalobainika katika sura hii ni kwamba mwingiliano wa jamii za mijini ulipokutanishwa na imani za kimila, ulionekana kuwa mgongano wa mila. Mila na utamaduni wa mjini umeambatana sana na amali za kigeni. Uchumi wa mijini unaoambatana sana na pesa, umeambatana sana na mambo ya uharifu na ukosefu wa maadili. Jambo

18. Gamba la Nyoka - Uk. 11

lilo ndilo linalosababisha kutoelewana baina ya wazazi na watoto wao; kwa jinsi watoto wanavyoyaingilia maisha ya mjini kwa pupa na hivyo kupuuza mamlaka ya wazazi wao kwao.

Katika riwaya nne tulizozipitia, mwandishi anaonyesha kuwa uhusiano kati ya utamaduni wa asili na njia mpya za maisha ya nyakati hizi za leo, unafanya huo utamaduni uwe kiini cha mabishano yanyoletwa na kutopatana kati ya muundo mpya wa uchumi na maisha ya jamii.

Utafiti uliofanywa katika mabadiliko ya kiuchumi, umeonyesha kuwa marekebisho yaliyofanywa katika harakati za kiuchumi yameleta mikinzano katika jamii na tamaduni, na kuwa hakuna njia maalum za kusuluhisha hali hiyo. Ukweli wa maisha ni kwamba, mifumo ya kiuchumi huwa ni baadhi ya sehemu badilifu mno katika jamii. Hii ni kwa sababu husaidia kuyatimiza matakwa ya binadamu katika nyanja zingine za kijamii.

Katika sura inayofuata tutakichunguza kipengee cha kisiasa na kuona ni kwa njia gani mfumo wa kisiasa huwaathiri wanajamii katika mahusiano yao.

## 5:0 Sura ya Tano:

### 5:1 Utangulizi:

Riwaya ya Rosa Mistika (1971) na Kichwamaji (1974) zinamulika maisha ya watanzania baada ya uhuru. Msanii anauliza kama ni kweli uhuru ulileta mafanikio yaliyotarajiwa. Anafanya hivi, kwa kuangalia athari za kikoloni kwenye siasa ya Tanzania huru.

Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979) kwa upande mwingine zinayachunguza jamii hii ya watanzania chini ya mfumo mpya wa kisiasa - yaani wa kijamaa.

Sura hii inadhamiria kuonyesha kwamba, vitendo vya wahusika wa Kezilahabi vina msingi wake sio tu katika mfumo wa kitamaduni. kielimu na kiuchumi bali pia wa kisiasa. Vitendo hivi ndivyo vinavyowatenganisha wanajamii.

### 5:2 Athari za Mfumo wa Kibepari:

Katika riwaya ya Rosa Mistika wazee na viongozi wenye mamlaka ni mazao ya mfumo wa kisiasa wa aina ya kibepari. Ingawa mwandishi hatuonyeshi kwa njia iliyo wazi nafasi ya viongozi katika riwaya hii kama anavyofanya katika riwaya ya Kichwamaji, yaelekea anatudokezea kwamba hana imani na viongozi wa kisiasa kutokana na vitendo vyao viovu. Kwa mfano mkuu wa Wilaya ambaye apaswa kuwahudumia wananchi kwa kuwa yeye ni mtumishi wa serikali, ndiye anayempeleka Rosa (kijana anayepaswa kuwa bintiye) kupumzika 'Beach'. Yeye haoni haya kumchukua binti wa wenyewe na isitoche mbele ya babake binti mwenyewe (uk. 70). Hiki ni kitendo cha aibu kinachotuonyesha jinsi viongozi walivyoukosea umma heshima.

Mwandishi anafafanua tabia ya watu kama hawa kwa maelezo

.../65

kuhusu Deogratias ambaye anarejelewa kwa kinaya kama 'Bwana Maendeleo' wa Mwanza. Hasira za mwandishi kuhusu watu kama hawa zinajitokeza wazi anaposema:

> Deogratias alikuwa mmoja kati ya wale wazee wanaojifikiria bado vijana. Wazee wanaopendelea kutembea na vitoto vidogo ... Wazee wanaomezea mate matiti ya mtoto mdogo. ... Akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili alikuwa bado akiwaandikia wasichana barua akisema, "Ninakupenda kama almasi ya Mwadui..." Huyu ndiye alikuwa Deogratias Bwana Maendeleo, mchumba wa Rosa (Uk.50-51).

Ni wazi kwamba mwandishi hana imani na watu kama hawa. Anawaona kama maadui wakubwa wa maendeleo. Hii ni kwa sababu wanafanya kinyume cha matarajio ya jamii. Wazee hawa wanatumia vyeo na pesa kupata chochote wapendacho. Hivyo, wao ni masalia sio tu ya mfumo wa kisiasa bali wa kiuchumi. Mifumo hii aghalabu huenda sambamba.

Viongozi hawa ndio wanaowapa vijana kama Rosa ujasiri. Hatima yake ni kwamba watoto hawaoni sababu ya kuwaheshimu wazazi wao. Vijana wanaishia katika kuwahamazisha wazazi kiasi cha kuwafanya wawakane (uk. 70).

Matendo ya viongozi kama hawa yanajitokeza wazi katika riwaya ya Kichwamaji. Hapa tunaelezwa kwamba wanaoshika hatamu za uongozi baada ya uhuru ni wale wenye elimu. Elimu hii ya kikoloni ni muhimu katika kazi kama za utawala, umeneja na kazi zingine za madaraka makubwa. Manase ni mfano mzuri wa watu kama hawa. Yeye ana elimu ya Chuo Kikuu inayomfanya

ashike hatamu za uongozi kama mkuu wa Wilaya. Kazimoto anatudhihirishia umuhimu wa warithi wa elimu ya kikoloni anaposema:

> Wakati huu uhuru ulikuwa
> umekwisha ingia. Jina la
> Nyerere likawa likiimbwa hata
> na watoto wadogo. ... Kina
> Manase wakawa watu waliohitajika
> sana ili kushika uongozi wa nchi (uk.15)

Kama tulivyoona katika sura ya tatu, elimu hii haikutengwa katika kumnufaisha mwafrika. Hata hivyo ilimwathiri sana. Wale viongozi walioshika hatamu za uongozi wanadhihirisha wazi jambo hili.

Manase, mkuu wa Wilaya, anaifanya ofisi ya umma mahali pa kutekelezea vitendo vyake viovu kama kuwatongoza wasichana na kuandikia barua zisizo rasmi. Nje ya ofisi yake tunakutana na watu mbalimbali walio na hamu ya kuonana na mkuu wa wilaya. Machovu waliyo nayo ni ishara kwamba wamemsubiri mkuu wa wilaya kwa muda mrefu. Zamu ya mzee ya kuingia ofisini inapofika, jambo la kushangaza linatokea. Mzee anafukuzwa kwake ni ishara kwamba warithi wa ukoloni-viongozi wamekengeuka kiasi cha kutowathamini wazee wao. Mfumo wa kisiasa wa kibepari 'umewafunza' kufikiri kwamba kijana mwenye cheo ni bora kuliko mzee maskini asiye nacho. Lakini, je, ni kweli kwamba manase hajui kuwa wazee hujikongoja kwa fimbo. Ukweli wa kitendo hiki ni kwamba mzee yuafukuzwa ili msichana fulani aingie ofisini. Pili aingia ofisini mara tu mzee anapofukuzwa (uk.7).

Mkuu huyu wa wilaya ni kielelezo cha viongozi wabaya katika muktadha wa riwaya. Mzee anapofukuzwa tunajiuliza kama kitendo hiki cha Manase ni halali. Ingawa kitendo hiki chaweza kupewa fasili tofauti, la muhimu ni kwamba twakiona

kufukuzwa kwa mzee kama ishara kuwa wazee wanatengwa sio tu na jamii na serikali yao bali pia na watoto wao. Mwandishi anasema:

> Mzee alipokuwa akitoka nje
> sikuona kitu kingine isipokuwa
> kwamba wazee walikuwa wakitukimbia.
> Uhusiano kati yao nasi ulikuwa
> ukikatika. Niliona wazazi wakiwakimbia
> watoto wao ambao sasa walikuwa kama
> simba (uk.7).

Viongozi kama hawa ni viongozi kwa jina tu bali si viongozi kwa maana halisi ya kazi waifanyayo.

Mbali na kuzaa viongozi dhaifu katika kazi yao, mfumo wa kisiasa wa kibepari ni msingi mkuu wa hali ya kitabaka iliyoko. Wenye uwezo wa kisiasa na kiuchumi ni warithi wa ukoloni na elimu yake ambao katika riwaya za Kezilahabi aghalabu ni vijana (wasomi-teule). Ufanisi wa Manase, magari, jumba, mpishi na vifaa vingine vya thamani kubwa unalinganishwa na ulitima wa wazee kikaoni. Mzee mmoja analalamika kwa kuwa uhuru anao, kazi anaifanya, lakini hapati haki yake. Anasema:

> Uhuru tumekwishapata. Zamani
> mkoloni alikuwa akitengeneza pesa
> kidogo kwa sababu alikuwa hataki
> tuendelee na alikuwa akituonea
> katika mambo mengi. Hii haikuwa
> nchi yao. Yote hayo tumeambiwa
> na wanasiasa. Sasa uhuru tume-
> pata, kwa nini serikali haiwezi
> kutengeneza pesa nyingi kila mtu
> awe tajiri (58-59).

Mzee huyu anaonekana kuwa na fununu juu ya maswala ya kisiasa na kiuchumi katika nchi yake. Anaelewa kwamba

ingawa uhuru wanao faida zake hazifurahiwi na jamii nzima. Kuna wale wanaojua uhuru kwa jina tu. Katika muktadha kama huu, uhuru ni faida ya viongozi na wakuu wa serikali. Kutotosheka kwa wazee na maelezo ya Kazimoto kuhusu tofauti hizi ni Ishara kwamba wazee hawawezi kukubaliana na maelezo ya vijana kama Kazimoto. Hali hii yatudhihirishia tofauti zilizoko za kimtazamo baina ya makundi haya mawili kuhusu swala la siasa.

Viongozi wa nchi huru wanaonyesha kukengeuka kwa sababu ya kasumba za kikoloni, hawawezi kuwa vielelezo bora kwa jamii yao. Inaelekea mwandishi anatueleza kuwa kosa la Tanzania kabla ya siasa ya ujamaa ni la viongozi. Jambo ambalo linatudhihirikia ni kwamba baadhi ya viongozi wa Tanzania wametambua kosa lao na kujaribu kulitafutia tatuzi - Azimio la Arusha. Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa tatuzi hili ni mambo ambayo tutajadili katika sehemu zifuatazo.

## 5:3 Azimio la Arusha:

Mohammed S. Khatib (1887) anatuainishia baadhi ya sababu za kimsingi zilizosababisha kuzaliwa kwa Azimio la Arusha. Mbali na sababu za kiuchumi na kijamii, sababu muhimu iliyochochea kuzaliwa kwa Azimio la Arusha ilikuwa ni Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na hatua za haraka zilizo-chukuliwa na serikali ya Zanzibar, chini ya uongozi wa Karume kati ya mwaka wa 1964 na 1967.

Ingawa Zanzibar haikutangaza hadharani mwelekeo wa sera na itikadi ya serikali na chama chake cha Afro-Shirazi Party, kauli ya kwanza ya karume alipoongea na wananchi katika mapambazuko ya siku ya mapinduzi ya Zanzibar, ilionyesha nia ya ujenzi wa taifa la usawa, haki na ujamaa.

F.E.M.K. Senkoro (1982) akilizungumzia swala hili

.../69

alionelea ya kwamba Azimio la Arusha lilinuia kutoa ufafanuzi wa siasa ya ujamaa na kujitegemea. Lilianzisha uzindushi wa ujenzi wa jamii mpya yenye misingi ya usawa. Siasa ya Azimio hilo ilionekana kama jibu mahsusi la mikinzano ya kiuchumi na kijamii nchini. Ilinuia kuuteketeza ubepari, ukabaila na unyonyaji wote kwa jumla. Hivyo kati ya mambo yaliyopigwa vita ni pamoja na majumba yaliyohodhiwa kibinafsi.

Riwaya ya <u>Dunia Uwanja wa Fujo</u> inasawiri 'fujo' za aina mbalimbali kama vile umalaya, wizi, uhalifu na ubinafsi. 'Fujo' hizi ni matokeo ya mfumo wa kisiasa wa kibepari. Mbali na haya tunashuhudia pia matokeo ya mfumo wa kisiasa unaokumbwa kumbo na mfumo mpya wenye misingi ya kijamaa.

Wakulima ambao aghalabu ni wahafidhina, ni tabaka lililo gumu kubadili mwenendo wake na kaida zake za maisha. Hivyo, inakuwa ni vigumu kwao kulipokea Azimio kwa urahisi. Kwa mfano, Mulele ambaye ana shamba la migomba lililostawi sana haoni sababu ya kuhamia kijijini.[9] Anapinga siasa ya ujamaa sio tu kwa sababu ni ngeni kwake, bali pia kwa sababu inadhamiria kumtenganisha na maisha yake ya kijiji. Wengine wanakatalia mbali siasa hii kwa sababu wanaiona kama hali inayowatenganisha na maisha yao ya vijijini waliyoyazoea.

Mikutano inaitishwa ili kuwashawishi watu kuipokea siasa ya ujamaa. Katika mikutano hii wanaeleza maana ya ujamaa kama siasa ya kukomesha unyonyaji na wanapoelewa na mkuu wa wilaya wanaonekana kutotosheka. Maswali yanayo-ulizwa mkutanoni na malalamishi hasa ya wazee, ni ishara ya mikinzano iliyoko baina ya tabaka hili la wahafidhina na lile la kizazi kibadilifu.

Kwa wanasiasa, inawawia vigumu kueleza Azimio hadi lieleweke kwa wananchi "wa kawaida", wajaribupo kulifafanua wanajikuta wanajipinga na wanapingana na wananchi. Ufafanuzi

9. Kezilahabi (1975) - <u>Dunia Uwanja wa Fujo</u>
Uk. 49

wao unawafanya baadhi ya wazee wafikiri kuwa Azimio limeletwa na wakubwa ili wao (wazee) wapate taabu. Kwa mfano, Mzee mmoja analalamika kuwa vijiji vinawafaa wafungwa.[10]

Yaelekea mwandishi atudokezea baadhi ya sababu za kukataliwa kwa siasa hii ya ujamaa. Mkuu wa Wilaya kumwamrisha mzee aketi ni ishara ya mabavu katika kuwafanya watu wakubali ujamaa. Mkuu wa Wilaya na mzee wanapaswa kuwa ndugu kulingana na mapendekezo ya siasa mpya. Kumkaripia mzee sio kumwonyesha usawa na udugu. Uhalisi wa mambo ni kwamba siasa ya aina hii haiwezi kuwa tatuzi la uhusiano wa kitabaka ulioko baina ya wazee wanaoishi vijijini na viongozi (vijana walioelimika), wanaoishi mijini. Viongozi hawa chambilecho Nyerere (1969) wapaswa kuelewa kwamba:

> Madhumuni ya wananchi katika jamii yatafanikiwa ikiwa viongozi watayatekeleza mamlaka yao kwa njia tulivu na thabiti kama inavyopendekezwa na taasisi za kijamii.[11] (tafsiri yetu).

Hivyo ikiwa viongozi na wanasiasa watazingatia ukweli wa kauli hii, basi mikinzano kati ya makundi haya mawili itasuluhishwa.

Kwa watu kama Tumaini ujamaa ni kitu kibaya sana. Azimio la Arusha linamwona kuwa mnyonyaji kwani anahodhi mashamba makubwa na anawaajiri wafanyakazi kwa malipo duni. Ijapokuwa kifo cha Tumaini chaweza kuchukuliwa kama sehemu tu ya matokeo ya fujo za duniani, kwa hakika kifo chake chatokana na harakati za kitabaka. Ni matokeo ya athari za juhudi za Azimio la Arusha za kuikata mirija ya unyonyaji.

Hivyo ili kuzuia hali kama hii kutokea tena Raid (1976:25) anasema:

10. Kama Nambari 9 - Uk. 173
11. Nyerere, J. (1969): <u>Nyerere on Sociolism</u>
    Uk. 52

> Unapokuwa na shida kama
> hizi, unaona haja ya elimu
> na haja ya kuwa na walimu
> bora wa ujamaa, na mbinu
> bora za kufunzia.[12] (tafsiri yetu)

Raid, hapa anapendekeza watu wafunzwe siasa hii na umuhimu wake swala ambalo Kezilahabi anakabiliana nalo katika riwaya ya Gamba la Nyoka.

## 5:4 Mapokezi ya Siasa ya Ujamaa:

Jinsi siasa ya ujamaa ilivyopokelewa na watanzania na athari zake kwao imemulikwa katika riwaya ya Gamba la Nyoka. Riwaya hii chambilecho Gibbe (1982) inahusu ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa nchini Tanzania. Mwandishi anajaribu kuainisha baadhi ya sababu za kupingwa kwa mfumo huu wa kisiasa. Wanakijiji wa Kisole na Bucho wanapinga ujamaa na vijiji vyake kwa sababu mbalimbali. Baadhi ya watu hawataki kuacha nyumba zao nzuri na kwenda kuishi katika vibanda vibovu. La muhimu ni kwamba wanakataa siasa hii kwa sababu inaletwa na wajukuu zao. Wazee wa kijiji cha Kisole wanaona kuwa elimu ndiyo inayoharibu vijana na kuwafanya waanze kuzua siasa zisizo na maana. Kwa mfano mzee mmoja anasema:

> Wanakijiji wenzangu ninalo jambo
> moja la kusema. Wakubwa wa nchi
> yetu wamesoma. Sisi hatukupata
> kufika shuleni. Tukumbuke kuwa
> hawa wanaotutawala leo ni watoto
> na wajukuu wetu. Lakini jambo
> la kusikitisha ni kwamba sasa
> wameota mbawa na wameruka na
> kutuacha sisi porini. Wameruka
> kwenda mbali wakijidai kusahau
> porini walikotoka, wazazi wanakoishi.

12. Raid, J. (1976): Problems of Implementation
Uk.25

> Sasa hatuishi kuambiwa, 'Oh
> vijumba vyenu vichafu'. ...
> Je, maji waliyokunywa wakati
> wakiwa vifaranga yalitoka wapi?...[13]

Malalamishi ya mzee huyu ni dhihirisho la namna wanakijiji hawa wanavyochukizwa na siasa hii. Mwandishi aelekea kutueleza kwamba wakulima hawakukataa ujamaa bali hawakupendezwa na jinsi viongozi walivyojaribu kuwasukumia mfumo ambao hawakuwa wameandaliwa kuufahamu lengo lake.

Viongozi chipukizi wanashindwa kutekeleza kisiasa maagizo yenye busara. Kwa mfano Mambosasa na Mamboleo ni vijana wanakijiji wa Bucho wenye nadharia nyingi za kisiasa. Wanapofika kwa mama Tinda wanasema:

> Kesho mnatakiwa wote kujenga
> nyumba zenu katika viwanja
> vyenu vipya. Hii ni amri ya
> serikali.[14] (msisitizo ni wetu).

Amri hii ya serikali inakataliwa na wanakijiji na ndiyo sababu inayowafanya kuitisha mkutano ambapo wanaamua kupigana hadi mwisho. Kukubaliana na ujamaa, hakuchukuliwi tu kama kitendo cha uoga, bali kama kukubali na kuamini mambo ya kitoto.

Kezilahabi anaonyesha bayana kwamba viongozi chipukizi waliposhindwa kutekeleza kisiasa mwito wa kuwashauri na kuwahimiza wananchi kuanzisha vijiji vya ujamaa, walitumia vitisho, marungu na bunduki.[15] Hatima yake ni kwamba watu wanapoteza maisha yao na wengine kuwa vilema. Wanabucho wanaohamishwa kwanza watarajiwa wawahamishe wanakisole. Utekelezaji huu wa ujamaa unaonekana kuwa na kasoro kwa vile unazaa uadui miongoni mwa wananchi. Viongozi hawa wanasahau kwamba wazee wanahitaji muda na elimu ya kuwafunulia

13. Kezilahabi (1979) - Gamba la Nyoka - Uk. 15-16
14. Kama nambari 13 - Uk.12
15. Kama hapa juu - Uk. 40

.../73

maana ya ujamaa, chambilecho Nyerere (1969:49):

> Ujamaa hauzuki tu ghafla
> kutoka 'jungu la kani'.
> Hata mapinduzi yaliyofanikiwa
> sana huacha uchungu, tuhuma
> na uhasama kati ya wanajamii.

Maneno haya ya Nyerere yanatudhihirishi muhimu wa kutekeleza ujamaa kwa njia taratibu. Kezilahabi aelekea kutuambia kwamba ujamaa unawajia watanzania kabla ya wakati wake. Anaona umuhimu wa kuwatayarisha watu kabla ya kuletewa mabadiliko. Hii ni kwa sababu, bila ya matayarisho twatarajia kuwepo na umwagikaji wa damu jambo ambalo ni la kuvunja moyo.

Hata hivyo kushindwa kwa wanyonge, ni ishara ya ushinde wa mfumo wa kijadi na kuzaliwa kwa mfumo mpya wa kijamaa. Kichwa chenyewe cha kitabu yaani "Gamba la Nyoka" kinatoa taswira yenye fununu za ushindi wa ujamaa. Hii ni kwamba nchini Tanzania, nyoka ameshakufa, lililobaki ni "gamba tu la nyoka" - maanake ni kwamba mfumo dhalimu wa kibepari umepigwa vita vikali na kwamba matatizo ya kuitekeleza yanayojitokeza ni kama gamba la nyoka ambalo likiondolewa, jamii ya kijamaa inayojengwa haitakuwa na jambo la kuistua tena.

## 5:5 Kimalizio:

Katika sura hii tumeona athari za mfumo wa kisiasa wa kibepari na nafasi ya viongozi waliorithi ukoloni kabla ya Azimio la Arusha. Hali anayoizungumzia hapa Kezilahabi ni kwamba, ingawa uhuru umepatikana, umewafaidi wachache tu. Wananchi wengi wangali katika hali ya ufukara ambao unawatumikisha kwa wafrika wenzao. Hali hii inasababishwa na viongozi chipukizi ambao ni tabaka la vijana waliosoma. Viongozi hawa wameshindwa kutekeleza wajibu wao kwa jamii

jambo ambalo linawafarakanisha na wazee wao. Ili kutatua matatizo ya uongozi na mikinzano inayotokana na hali hii mwandishi ameonyesha jinsi nchi ya Tanzania ilivyoanzisha Azimio la Arusha.

Haya anayazungumzia katika Dunia Uwanja wa Fujo. Ujamaa unapotolewa kwa wakulima, wanaukataa kwa kusingiziwa itikadi na siasa wasioifahamu. Pengo lililopo kati ya serikali inayotaka kuleta ujamaa na wakulima wanaotarajiwa kuutekeleza ni kubwa mno. Mwandishi ameonyesha udhaifu wa utekelezaji wa mfumo huu mpya. Matumizi ya vitisho badala ya mjadala ni jambo ambalo linasababisha chuki kati ya wanajamii. Wazee wanawalaumu watoto wao kwa kuleta siasa wasioielewa.

Anachokisema Kezilahabi katika riwaya hii ni kwamba mikinzano hii imetokana na ukweli kwamba viongozi chipukizi hawatoi maelezo ya kumridhisha mkulima kuhusu haja ya kuleta mabadiliko. Hivyo, wanashindwa kuutekeleza ujamaa kwani wakulima hawawezi kushawishika kwa nadharia tupu.

Lengo la mwandishi katika riwaya ya Gamba la Nyoka kama ilivyo katika Dunia Uwanja wa Fujo ni kuonyesha kuwa utekelezaji wa ujamaa nchini Tanzania una ugumu wake. Tumeona kwamba kama wananchi hawatatayarishwa kuupokea, kupitia kwa elimu na maelezo ya kuridhisha, basi tatarajie mikinzano inayowatenganisha wananchi sio tu na serikali yao bali pia na wananchi wenzao. Riwaya hii inaonyesha mabadiliko ya Tanzania kutoka hali moja hadi nyingine. mabadiliko haya yanamithilishwa na mnyumbuko wa nyoka ndiposa anwani yake, "Gamba la Nyoka". Ni maoni ya tasnifu kwamba nia ya mwandishi katika kitabu hiki sio kutwambia kuwa ujamaa umeshapatikana. Kinatwambia tu kwamba, wanakijiji wamo ndani ya kijiji na hiyo ni hatua ya mwanzo tu ya ujenzi wa ujamaa.

## 6:0 SURA YA SITA:

### 6:1 Hitimisho:

Katika kazi hii tumejaribu kuangalia jinsi Euphrase Kezilahabi, mwandishi wa riwaya za Rosa Mistika (1971), Kichwamaji (1974), Dunia Uwanja wa Fujo (1975) na Gamba la Nyoka (1979), alivyolisawiri swala la bonde la wakati. Tumefanya hivyo kwa kuzingatia zaidi maudhui ya riwaya hizi na jinsi wahusika wanavyosawiriwa. Kutokana na hayo yote maoni ya mwandishi kuhusu mambo kadhaa yanajitokeza.

Katika kulijadili swala la malezi yaelekea kwamba utamaduni wa jadi unashindwa katika kujenga maadili ya vijana. Tunadai hivi kwa sababu malezi yaliyo na misingi yake katika aina hii ya utamaduni yanakuwa kiini kikubwa katika kuzua migogoro kati ya kizazi kipya na kikongwe. Vijana wanakua katika wakati wa sasa ambao ni tofauti na ule wa zamani kwa sababu ya maingiliano ya jamii mbalimbali. Maingiliano haya yameleta kuathiriana kwa tamaduni mbalimbali ambako kumezusha matatizo tofauti na yale ya jadi.

Mwandishi anapomsawiri Rosa kama mhusika anayeishi maisha yaliyojaa taabu na hatimaye kutengana na babake, anaishutumu jamii ambayo imeshindwa kumwelekeza Rosa na vijana wengine kwa kuwapa malezi finyu yaliyo na misingi yake katika ujadi. Mfumo wa malezi katika utamaduni jadi wahitaji kufanyiwa marekebisho ambayo yatawafanya vijana kuwaelewa wazazi wao na hivyo kuishi katika hali ya kutangamana.

Kutoroka kwa Anastasia katika riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo, ni ishara kwamba mwandishi anapinga ndoa ya kulazimishwa - yenye misingi katika utamaduni jadi. Kitendo cha Anastasia chalingana na kile cha Riziki mhusika wa

.../76

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

J. Kitsao (1980). Yaelekea waandishi hawa wanawaeleza wazazi kuwa, kuwaoza binti zao kwa wazee kwa sababu ya mahari hakuna nafasi katika dunia ya leo. Wasichana wanapaswa kupewa uhuru wa kuchagua wachumba wawapendao. Isitoshe, swala la mahari mapenzi na furaha ya msichana, Hivyo, jamii ikiendelea kuwalazimisha wasichana kuolewa na wazee basi tuwe tayari kupambana na uasi wa kina Anastasia, Tumaini na Dennis wa Kezilahabi ambao hatima yake ni mikinzano kati ya kambi ya vijana na ile ya wazee.

Hivyo katika tasnifu yetu imebailika kwamba utamaduni ndicho kiini hasa kinacholeta migogoro inayosababisha bonde la wakati.

Kuhusu nafasi ya dini, yaonekana imeshindwa kuzitatua shida zinazoikumba jamii. Hii ni kwa sababu inayapuuza maisha halisi ya hapa duniani. Ukweli wa kauli hii unaungwa mkono na nadharia ya uyakinifu wa kisoshiolisti ambayo huchukulia maisha kuwa ni vitendo. Kinyume na mwelekeo wa dini unaopendekeza maisha bora ya mbinguni, nadharia hii huzungumzia raha kuu ya kuishi ulimwenguni ambayo lazima binadamu afanye awezalo kuilinda ili kuweza kuishi kama muungano wa jamii moja ya kibinadamu.

Kulingana na nadharia ya Uyakinifu wa Kisoshiolisti lazima mwandishi aonyeshe uwezo wa mwanadamu wa kubadilisha hali yake ya maisha kuwa bora zaidi. Hii ni kwa sababu nadharia hii yashikilia kwamba mwanadamu ana uwezo wa kubadilisha hali yake na kuifanya iwe bora zaidi. Akilizungumzia swala hili Reiss (1978:150) anasema:

> Ili kutoa uhakiki imara kuhusu
> jamii msanii sharti awe mweledi

> wa uwezo wa mwanadamu wa
> kuudhibiti ukweli pamoja
> na kuudhibiti ulimwengu
> na kuubadilisha uhusiano
> wa kibinadamu na kijamii.
> (tafsiri yetu).

Kuhusu athari za elimu ya kikoloni mwandishi anaiona elimu hiyo kama chombo kinachovitenganisha vizazi katika jamii. Hii ni kwa sababu mkabala wa jamii umekuwa kwamba mtu huwa wa maana akiwa na cheo cha juu tu - yaani akiwa na elimu. Hali na imani hii imeleta mgongano mkubwa na kuwasilisha upotofu kama ule tuliouona kati ya Manase na mzee au vijana wanamapinduzi, Mambosasa na Mamboleo wa Gamba la Nyoka.

Nadharia ya uhalisi wa kisoshiolisti inasisitiza kwamba mabadiliko hayana budi kufanywa pale inapohitajika. Mwandishi aelekea kupendekeza mabadiliko ya vyombo vyote kama vile elimu, vinavyoathiri mgongano wa aina hiyo. Madhumuni ya elimu hupatikana kutokana na hamu ya kufanikiwa katika kupita maarifa ya ujuzi unaohitajika. Jambo analotukumbusha mwandishi ni kwamba maarifa na ujuzi ni swala la kando sio lengo muhimu katika mfanyiko huo. Maarifa anayopata mtu lazima yaende sambamba na harakati za kila siku hasa za kiuchumi, kikazi na kijamii. Tabia pia lazima itiliwe mkazo iwapo harakati za jamii kwa jumla zitaimarishwa. Jambo hili litaweza kuziba tofauti zilizopo kati ya wanajamii na hivyo kuwa na msingi bora wa maendeleo. Kwa njia hii tumeweza kubainisha kuwa katika riwaya za Kezilahabi elimu imemulikwa kama kiini muhimu kitetacho utengano unaosababisha bonde la wakati.

Inaonekana kwamba elimu ya kikoloni ambayo imemtenganisha msomi na jamii yake na kukifanya kizazi kimoja kukidharau kizazi kingine haimfurahishi mwandishi. Tabia za wasomi

wa elimu hiyo hazionekani kumpendeza mwandishi. Kudhoofika kwa tabia za wasomi kuna msingi wake katika swala kwamba, elimu ya kikoloni imeambatana na utamaduni mpya ambao unaifanya elimu hiyo kuwa sababu ya utengano kati ya vijana na wazee.

Mojawapo ya haipothesia zetu ilikuwa kwamba masiala ya kiuchumi - jamii ni sababu kubwa ya migogoro inayosababisha bonde la wakati. Jambo hili limebainika katika sura ya nne. Tumeweza kubainisha kwamba uchumi wa mijini unaoambatana sana na pesa umeambatana pia na mambo ya uhalifu na ukosefu wa maadili. Mwandishi anaonyesha kwamba uhusiano kati ya utamaduni anaonyesha kwamba uhusiano kati ya utamaduni wa asili na njia mpya za maisha ya nyakati hizi za leo, unaufanya huo utamaduni uwe kiini cha mabishano yanayoletwa na kutopatana kati ya muundo mpya wa uchumi na maisha ya jamii. Hii inaungwa mkono na nadharia ya uyakinifu wa kisoshiolisti inayohimiza kwamba kila tukio katika historia ya mwanadamu halitendeki tu kwa bahati bali lina sababu zake zenye misingi katika uhusiano wa kijamii na kiuchumi.

Kwa kiasi fulani imebainika kwamba siasa pia ni mojawapo ya kiini kinacholeta utengano unaosababisha bonde la wakati. Hili limejitokeza pale ambapo mwandishi anapousawiri udhaifu wa viongozi chipukizi wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao kwa jamii jambo ambalo linawafarakanisha na wazee wao. Tumeona kwamba lengo la mwandishi katika riwaya zake mbili yaani Gamba la Nyoka (1979) na Dunia Uwanja wa Fujo (1975) ni kuonyesha kuwa utekelezaji wa ujamaa nchini Tanzania una ugumu wake. Mwandishi anatuonyesha ukweli wa mambo kwamba, kama wananchi hawatatayarishwa kuupokea, kupitia kwa elimu na maelezo ya kuridhisha, basi tutarajie mikinzano inayowatenganisha wananchi sio tu na serikali yao, bali pia na wananchi wenzao.

## 6:2 Uanafalsafa wa Kezilahabi

Kezilahabi ni mwandishi anayetazama masuala mengi na katika vipengele vingi. Katika riwaya nne tunazozihakiki Kezilahabi anayazungumzia matatizo halisi yanayoikumba jamii yake. Kama wasanii wengine anayatumia matatizo ya jamii yake kama malighafi ya kuziundia kazi zake. Hilo ni jambo ambalo apaswa kupongezwa kwalo.

Wahakiki wengi wa kazi za Kezilahabi mathalani Senkoro (1982), Mulokozi (1983), Musau (1985), Lugano (1989) na wengineo wameiona falsafa ya mwandishi kuhusu maisha kuwa ya kukatisha tamaa. Senkoro kwa mfano anasema kuwa:

> Maisha kwa kufuatana na E.
> Kezilahabi hayana maana
> kwani ni tanzia tupu.[1]

Hii ni kwa sababu wanaposoma kazi za mwandishi huyu wanaona wahusika wengi wakifa. Jambo ambalo mwandishi huyu anatumulikia ni kuwa maisha yamejaa "fujo" za aina nyingi. 'Fujo' hizi zinawafanya wanadamu kukata tamaa. Mifumo ya elimu, utamaduni, uchumi na siasa inakatisha tamaa kwa sababu ya jinsi inavyokuwa kiini cha mikinzano katika jamii. Hii si kusema kwamba mwandishi haoni matumaini katika jamii yake katika siku zijazo bali alichofanya ni kujikita katika kuonyesha uozo wa jamii. Kezilahabi ana msimamo maalum wa kuonyesha madhara yanayozaliwa na mifumo hiyo.

Hata hivyo ingawa anaumulika uozo wa ulimwengu mtazamo wake unapingana na falsafa ya uyakinifu wa kisoshiolisti. Hii ni kwa sababu mtazamo huo unayatenga

1. Senkoro, F. (1982): Fasihi, Publicity Press Centre. Uk. 89

matukio kama vile uzinifu, uasi, umalaya n.k. pamoja na maisha ya watu kama vile Rosa, Anastasia n.k., na uhusiano wa kijamii na kiuchumi kama asemavyo Mulokozi.[2]

Kwa kuyatenganisha matukio na mazingira yake ya kiuchumi, kielimu, kijamii na kisiasa, mwandishi anayaona maisha kama kitu kisicho na nidhamu wala kanuni. Mtazamo huu wa mwandishi ni kinyume cha mtazamo wa uyakinifu wa kisoshiolisti, unaoshikilia kwamba maisha ya mwanadamu yanayotawaliwa na sheria fulani, Lukačs (1962:2), za kiuchumi na kijamii katika wakati maalum wa kihistoria. Kwa mujibu wa mtazamo huo, matukio katika jamii yanaweza kueleweka kwa muktadha wa uhusiano wa kiuchumi na kijamii katika historia ya mwanadamu. Tukichukua tatizo la vijana wanaopinga ndoa za kulazimisha, kwa mfano, tutaona kwamba vijana hao wana sababu halisi za kijamii zinazowafanya kuzipinga ndoa hizo. Mojawapo ya sababu hizo ni ukweli kwamba wakati umebadilika na hivyo jamii haina budi kubadili mitazamo yake kulingana na mapito ya wakati. Vijana na wazee wana mielekeo tofauti kuhusu masiala ya kijamii jambo ambalo linazusha kutoelewana kati yao.

Hata maisha ya Rosa yana sababu halisi za kihistoria zinazotokana na uhusiano wa kiuchumi na kijamii katika jamii yake. Mgongano wa Rosa na babake kama tulivyoona katika sura ya pili, ni mgongano wa bonde la wakati. Rosa analisimamia kundi la vijana wanaopinga maisha yenye mielekeo ya kijadi.

Mtazamo wa mwandishi unaoyaona maisha kama 'fujo' unatufanya tuione historia ya mwanadamu kama kitu ambacho hakina mwelekeo na ambacho kimesimama mahali pamoja. Msimamo kama huo tunaupinga kwa kuwa twajua kwamba historia ya mwanadamu inabadilika kutoka hali moja ya uzalishaji mali hadi nyingine chambilecho Mulokozi (1983:11):

2. Mulokozi, M. (1983): <u>Kiswahili</u>: Jarida la T.U.K.I Toleo 50/1 Uk. 4

.... jamii inakua na kubadilika
kihistoria toka hali ya chini
na duni kuingia katika hali ya
juu ya kijamii ....

Hivyo historia ya jamii haisimami mahali pamoja kama anavyoiona Kezilahabi, bali inabadilika na ina mwelekeo.

Katika utangulizi wa tasnifu hii tulidai kuwa, jukumu mojawapo la fasihi ni kuieleza, kuichambua na kuikosoa jamii katika kuleta mabadiliko yafaayo ndani yake. Kwa mujibu wa kauli hii tunaamini kuwa Kezilahabi analitimiza jukumu hili kwa kuwa anaumulika uozo wa jamii kwa jicho pevu.

Mijadala anayoibusha Kezilahabi kuhusu masiala ya dhana ya raha, ukweli na maana ya maisha yanamweka katika tapo la wanafalsafa wa aina yake. Hivyo, kuna haja ya kumsoma na kumhakiki Kezilahabi kwa jicho la kutathmini kwa undani zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Katika mahojiano kati yake na mwandishi wa Kiswidi Las Bernander (1978), Kezilahabi amekiri ya kwamba, aliathirika kiasi kikubwa na maandishi ya wana-utamaushi Backet na Camus. Athari hizi zinajitokeza wazi katika maandishi yake hasa kwa jinsi anavyowaumba na kuwasawiri wahusika wake. Vile vile utatuzi wa matatizo yanayowakabili wahusika wake kila siku umefungamana sana na mtazamo huu wa kifalsafa.

Ingawa Kezilahabi anajadili matatizo ya jamii yake kwa ubingwa mkubwa, mtazamo wake ambao umeathiriwa na falsafa ya utamaushi hauonekani kuleta mafanikio yoyote katika siku zijazo. Hii ni kwa sababu hujaona maisha ya mwanadamu kama kitu kisichobadilika. Kinyume na mwelekeo wa mtazamo wake Kezilahabi tumeonyesha kwamba kila tukio la maisha ya binadamu lina asili yake katika mahusiano ya

binadamu na mazingira yake. Hivyo, shida ya bonde la wakati kama matatizo mengine katika jamii yana msingi wake katika mifumo ya kijamii na kiuchumi.

6:3 Ukuaji wa Mwandishi Kifalsafa:

Katika riwaya zake za hivi karibuni Nagona (1990) na Mzingile (1991), Kezilahabi anashughulikia masiala ya ukweli wa maisha. Riwaya hizi ni mazao ya kifasihi ambayo yanaweza kusemekana kuwa yanatokana na kile J.S.Madumulla(1987) anachokiita visaasili mambo-leo ambavyo vinaonyesha kifalsafa maendeleo ya mzunguko ambao mwanadamu anafanya pasipo kuweza kufika katikati ya mzunguko huo ambapo pana ukweli wa maisha. Riwaya ya Nagona inaeleza matatizo ya dunia yaliyozushwa na mchangamano wa mataifa ulimwenguni; matatizo yanayoendelea bila kukoma na bila sulubu kwa sababu elimu ya kweli ya utatuzi wake haijapatikana na labda haifapatikana kwa muda mrefu ujao.

Madumulla (op.cit) anasema kwamba mwelekeo wa Kezilahabi katika Nagona ni wa kisaasili na unaweza kulinganishwa na wa Christa Wolf katika Cassandra riwaya inayoeleza kuangamia kwa Ugiriki.

Swala moja muhimu linaloibuka katika riwaya hizi ni kuhusu suluhisho la matatizo ya mwanadamu. Haieleweki kama litatokana na itikadi za kidini au aina fulani ya maarifa.

Riwaya ya Mzingile yaelekea kuendeleza fumbo kuhusu Mungu ambalo liliibushwa katika Nagona. Yaelekea maisha yamekosa maana yoyote kwa vile binadamu hana uwezo wa kuyaelewa au hata kumwelewa Mungu ni nani. Hii yatokana na kutoweza kwa binadamu kuelewa ukweli wa maisha.

Jambo linalojitokeza katika riwaya hizi mbili ni kwamba suala la dhana na maana ya maisha linalozungumzwa katika riwaya zingine nne za kwanza, ndilo linaloendelezwa katika riwaya hizi mbili ambazo zaweza kuchukuliwa kama 'mapacha'[3] katika jinsi zinavyoshahibiana kwa dhamira zake zinazochambua suala gumu la kifalsafa lihusilo maana ya maisha.

Tofauti na riwaya zingine, swala hili limekabiliwa kwa mwelekeo wa kifalsafa zaidi kuliko katika riwaya za awali.

Nagona na Mzingile ni riwaya pevu zinazohusu fumbo la kifalsafa kuhusu nini maana ya maisha. Swala la jinsi waandishi wengine walivyomwathiri Kezilahabi halijashughulikiwa kwa undani. Tunaamini kuwa iwapo jambo hili litafanywa litawawezesha wasomaji wa Kezilahabi kumwelewa kwa njia iliyo wazi.

Kufikia hapa hatuna budi kujiuliza umuhimu wa kazi hii. Twadhani kwamba kwa vile tahakiki hii ni kazi ya fasihi ya Kiswahili, basi tumeongeza mchango wetu katika kuikuza fasihi hiyo. Tunaamini pia kwamba, mbali na kuonyesha mwelekeo wa mwandishi na jinsi anavyoiona jamii yake anayoiandikia, kazi hii imewafunulia wasomaji wa Kezilahabi uandishi wake. Isitoshe, kazi hii imejaribu kuonyesha kuwa nadharia ya uyakinifu wa kisoshalisti inaweza kutumiwa kama kigezo cha kuipimia kazi ya kifasihi ili kuonyesha umuhimu wa kazi hiyo kwa jamii.

Ingawa tumejaribu kuzihakiki riwaya nne za Kezilahabi kimaudhui, na kuonyesha jinsi mwandishi alivyolisawiri suala la bonde la wakati, kuna mengine ambayo yanahusiana na kazi hizi ambayo hatukuyashughulikia kwa sababu ya upeo wa kazi yetu.

Jambo mojawapo linaloweza kuangaliwa na wahakiki wengine ni jinsi nadharia za kimtindo zinavyoweza kutumiwa katika

3. Maelezo haya tuliyanakili kutoka jalada la riwaya ya Nagona (1990)

.../84

kuzihakiki riwaya za Kezilahabi.

Pia lingekuwa jambo la maana kuzilinganisha kimtindo riwaya za Nagona na Mzingile na riwaya za awali. Jambo hili litaonyesha vile mwandishi alivyoendelea kimtindo.

**MAREJELEO:**


Chacha N. Chacha (1986) "Mazingira ya Mwanamke katika Fasihi ya Kiswahili. Makala katika Mwamko Toleo la 3, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Erikson, E. H. (1961) Youth: Change and Challenge. Basic Books Inc. Publishers, Newyork.

Frantz, F. (1970) Black skins White Masks. Grove Press, NewYork.

Gachukia, E. (1980) Cultural Conflict in East African Literature. Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu, Nairobi.

Gibbe, A. G. (1982) "Baadhi ya Taswira katika Gamba la Nyoka". Makala katika Kiswahili Toleo la 49/1. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Habwe, J. H. (1987) "Kezilahabi kama mwandishi wa Kisiasa". Tasnifu ya B.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Hussein, E. (1970) Wakati Ukuta. East African Publishing House Nairobi.

Iliffe, J. (1971) Agriculture Change in Modern Tanganyika. East African Publishing House, Dar es Salaam.

Kenyatta, J. (1961) Facing Mount Kenya. Mercury Books, London

Kezilahabi, E. (1971) Rosa Mistika. East Africa. Literature Bureau, Nairobi.

_______________ (1974) Kichwamaji. East Africa Literature Bureau Dar es Salaam

_______________ (1975) Dunia Uwanja wa Fujo East African Literature Bureau, Nairobi.

_______________ (1979) Gamba la Nyoka. East African Publishing House Dar es Salaam.

_______________ (1990) Nagona. Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

_______________ (1991) Mzingile. Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam

Kitsao, J. (1981) Uasi. Oxford University Press, Nairobi

_______________ (1975) "A stylistic Approach Adopted for the study of Written Swahili Prose Texts." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

_______________ (1982) "An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to chosen Texts." Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Lugano, R. S. (1989) "Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Lucaks, G. (1962) The Meaning of Contemporary Realism. Merlin Press, London

Madumulla, J. S. (1987) "Maendeleo ya Wahusika katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania." Makala katika Jarida la Kiswahili Juzuu 54, Dar es Salaam.

Mckee, J. (1969) Introduction to Sociology Holt Rinehart and Wilsten Inc., New York.

Mlacha, S. A. K. (1988) "Effects of Foreign Culture to the Younger Generation: A case study of Kezilahabi's Three Novels." Makala katika Jarida la T.U.K.I. Kiswahili Juzuu 55/1 & 2 Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mohammed S. Khatib (1987) Mulika. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Toleo No.19 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Mulokozi, M. (1976) "Fasihi na Mapinduzi" Makala katika Kioo cha lugha, Jarida la chama cha Kiswahili Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

__________ (1983) "Dunia Uwanja wa Fujo" Makala katika Kiswahili Toleo la 50/1. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Musau, P. M. (1985) "Euphrase Kezilahabi Mwandishi aliyekata Tamaa." Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwanyika, E. (1978) "Silika na Mazingira katika Kumuumba Rosa Mistika." Makala katika Kioo cha lugha Toleo la 7. Chama cha Kiswahili, Chuo cha Dar es Salaam.

Musgroove, F. (1964) Youth and the Social Order. Routledge and Kegan Paul Ltd., London.

Ngara, E. (1985) Art and Ideology in the African Novel. (A study of the influence of Marxism on Africa writing). Heinemann Educational Books Ltd., Nairobi.

Ngugi wa Thiong'o (1978) Homecoming. Heinemann Educational Books Ltd. Nairobi.

Nyerere, K. (1969) Nyerere on Socialism Oxford University Press Dar es Salaam.

__________ (1985) Education for Self Reliance. Government Printers, Dar es Salaam.

Ohly, R. (1981) Aggressive Prose. Institute of Swahili Research, Dar es Salaam.

Omari, C.K. na Mvungi (1981) Urithi wa Utamaduni Wetu. Mitaala ya Lugha na Fasihi No.9 Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Ortega, Y.G. (1933) Man and Crisis En torno a Galileo Norton, New York.

Raid, J. (1976) Problems of Implementation (Experiences from West Lake Region) University of Dar es Salaam Research Report No. 10.


UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY

Reiss, H. (1978) The Writer's Task from Nietsche to Brecht. The Macmillan Press, London.

Rodney, W. (1972) How Europe Underdeveloped Africa. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Samora, M. (1977) Establishing People's Power to serve the Masses. Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (1976) "Utamaduni Katika Riwaya ya Kiswahili." Makala katika Jarida la T.U.K.I. Kiswahili Toleo la 46/2 Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

__________ (1982) Fasihi. Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.


UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY